Vraag niet om oorlog, verspreid geen aids

Utakufa kifo mwili mifupa pekee

Je zult sterven, je lijf, je botten, in eenzaamheid

4.

Gonjwa la ukimwi latupunguza jamani

De ziekte aids dunt onze bevolking uit, mensen

takwimu ya watu yawa ni hati punguzo

de statistieken hierover bewijzen dat

Watoto yatima oneni walivyozi

zie hoe het aantal wezen toeneemt

hawana walezi wazazi wameshalala
 ze hebben geen opvoeders, ouders zijn al ingeslapen
Oneni wenyewe jamaa na ndugu zetu
 Zie hoe bij je familie en vrienden
Wanavyoanguishwa kwa gonjwa hili ukimwi
 door deze ziekte aids mensen al zijn omgekomen
japo tunasema eti kufa ni kulala
 en dan zeggen we nog dat sterven hetzelfde is als slapen
kufa kwa ukimwi heri ungongwe na gari
 je kunt nog beter door een auto overhoop gereden worden dan te sterven
 aan aids

5.

Mila desturi tunazozindekeza
 Zeden en gewoonten die we koesteren
katika jamii zaenda kutumaliza.
 In onze samenleving, richten ons te gronde
Kurithi wajana na kutakasa vilio
 het erven van weduwen en het reinigen van lijken
ni hatari sana wananchi tuepuke
 is heel erg gevaarlijk, laten we dat vermijden medeburgers
Kuoga ziwani mtoni ukiwa uchi
 naakt baden in meer en rivier
tuepuke sana tupunguze vishawishi
 laten we dat echt vermijden opdat we de verleidingen weerstaan
Kutoga kuchanja kutahiri kwa foleni
 Piercings, snijden, circumcisie
kuna sababisha kuenea kwa virusi
 veroorzaken verspreiding van het virus
tunawaomba, tunawaomba, tunawaomba watanzania
 wij smeken jullie, wij smeken jullie, wij smeken jullie, Tanzanianen
ndugu zetu tunawalilia, tunawalilia, tunawalilia
 we huilen, we huilen, we huilen om onze vrienden
waliokwsha mezwa na joka ukimwi
 die al door de slang aids opgeslokt zijn
kina baba tunawaomba, tunawaomba, tunawaomba kwa Mungu
 wij bidden, wij bidden, wij bidden voor iedereen tot God

Lied 7

Tishio la ulimwengum ‘Bedreiging van de wereld’

1.

Tishio la ulimwengu ni ugonjwa hatari

De bedreiging in de wereld is een gevaarlijke ziekte

Wazidi kupamba moto duniani

Deze verspreidt zich als een vuur in de wereld

Wataalamu wamekaa kujadili kinga

Experts hebben gediscussieerd over bescherming

Ya Ukimwi lakini imeshindikana

tegen aids, maar ze zijn er niet in geslaagd

Ukimwi hauna dawa wala hauna kinga

Er zijn geen medicijnen of bescherming tegen aids

Jiepushe na sindano mitaani

Vermijd het gebruik van spuiten op straat

Usherati, urawiti kuchanjana na nyembe

Vermijd overspel, vuiligheid, snijden met mesjes

Jiepushe mwananchi uokoke

vermijd dat, burger, zodat je gered wordt

2.

Adui huyu ukimwi chukizo kula wote

Deze vijand, deze huiveringwekkende aids, verslindt iedereen

Ameuzuwa ugomvi duniani

Hij heeft veel strijd in de wereld gebracht

Tazama katika kaya ndugu na jamaa

Kijk in ieder huishouden bij vrienden en familie

Wametengana kwa sababu ya ukimwi

ze gaan uit elkaar door aids

3.

Adui huyu ukimwi ni mchonganishi

Deze vijand, aids, zet mensen tegen elkaar op

Pia kufanya watu kutoelewana

Ook zorgt aids er voor dat mensen elkaar niet begrijpen

Akishafika nyumbani hupumbaza watu

Als aids al binnengekomen is, verblindt het mensen

Watu hushika imani za kurogwa

Mensen geloven in witchcraft

Fulani ndiye mchawi ana macho mekundu

Fulani, die tovenaars, heeft rode ogen

Twendeni sasa kwa maganga Sangagwena

Laten we naar dokter Sangawena gaan

Atupigie ramli tujue aliyeroga

Hij voert een sessie met ons uit zodat we weten wie magie op ons uitvoert

Tumkate kwa mapanga awawe

laten we hem met de hakbijl doden

4.

Ndugu yangu sikiliza unapougua ni muhimu

Mijn vriend, luister, wanneer je ziek bent, is het belangrijk,

Uende kwanza ukapime

Dat je je eerst laat testen

Ukibaini tatizo linalokusibu

zodat je weet welke problemen er zijn

Utajua ufanye nini uokoke

en je weet wat te doen om te overleven

Vipimo kitu cha kwanza twendeni

Testen is het eerste wat gedaan moet worden, laten we gaan

Tukapimwe tutambue afya zetu wananchi

laten we een test uitvoeren zodat we onze gezondheidstoestand kennen, burgers

Zuia ukimwi sasa: sema ukimwi basi

vermijd aids nu: zeg nu is het klaar met aids

Timiza ahadi yako wajibika

hou je aan de belofte zoals je die aan elkaar gegeven hebt

5.

Takwimu zinaonesha hapa Tanzania

De statistieken tonen hier aan in Tanzania

Maabukizo ya ukimwi yako juu

dat de aidsbesmettingen hoog zijn

Kumi na tatu pasenti ya maambukizo

13 % besmetting

Yako mkoani Mbeya namba one

in het Mbeya district, dat daarmee nummer een is

Namba mbili ni Mtwara ni hatari

nummer twee is Mtwara, gevaarlijk

Nambari kumi na nane ni namba ya Mara

Mara staat op de achttiende plaats

Katika maambukizi kitaifa

van de nationale besmettingen

Hivyo jama tujilinde na tuogopane

Daarom, vrienden, laten we ons beschermen en laten we bevreesd zijn

Tusiyafanye mapenzi kihohela

Laten we geen verwerpelijke liefde bedrijven

Lied 8

Usia kwa wanafunzi ‘Advies voor leerlingen’

1.

Wanafunzi wa shule za sekondari

Leerlingen van de middelbare school

Na msingi jamani mnashangaza

en van de lagere school, jullie roepen verbazing op

Wanafunzi hivi mmekuwaje

leerlingen jullie zijn nu aan het groeien

Mwashangaza tena mwasikitisha

Jullie veroorzaken verbazing en verdriet

Mwajifanya eti mmeshakua

met de nukken die jullie vertonen, wel jullie

Kumbe ninyi bado ni vifaranga

hebben al veel verbazing opgeroepen, jullie zijn nog kuikentjes

2.

Wanafunzi ninyi bado ni watoto

Leerlingen jullie zijn nog kinderen

Tena bado mwaogea kwenye dishi

jullie baden nog in een kinderbadkuip

Kubalehe siyo kwamba mmekua

Puberen betekent nog niet dat jullie volwassen zijn

Kuvunja ungo siyo mmekua

Menstrueren betekent nog niet volwassen zijn

Na kuota matiti siyo kukua

het krijgen van borsten betekent nog niet volwassen worden

Ninyi bado ni makinda ya kutishwa

jullie zijn nog kuikentjes die bedreigd worden

3.

Wanafunzi kuweni waadilifu

leerlingen handel moreel juist

Msifanye mapenzi mtaumbuka

bedrijf geen beschamende liefde

Mwajiponza kwa kauli mitaani

Jullie brengen jezelf in gevaar door jullie manier van praten op straat

Mnasema ponda mali kifo chaja

men zegt: geld verspillen is als de dood kopen

Siyo siri wanafunzi mnatisha

het is geen geheim, leerlingen, dat jullie een bedreiging vormen

Kwa mapenzi mitaani mwaongoza

door de liefde die jullie op straat bedrijven

4.

Wanafunzi jamani twawausia

Leerlingen, vrienden, wij geven jullie advies

Msiige matendo ya wakubwa

boots niet het gedrag van volwassenen na

Ya wakubwa yaachenii wayafanye

laat de gedragingen van volwassenen achterwege

Mkifanya mtapasuka misamba

als jullie dat doen breken jullie je kruis

Na mapenzi ni sumu yenu watoto

en liefde is gif voor jullie kinderen

Jichungeni msinaswe na miwaya

doe het niet verander: let op zodat jullie geen aids krijgen

5.

Mkifanya mapenzi umri wenu

Als je liefde bedrijft op jullie leeftijd

Mtakumbwa na madhara ya maisha

zullen jullie ten onder gaan en het leven verliezen

Mkimimbwa mtafukuzwa shuleni

als jullie zwanger worden, zullen jullie van school gestuurd worden

Mtamimbwa mtatengwa na jamii

als jullie zwanger worden, zullen jullie uit de familie verstoten worden

Mkifanya mapenzi umri wenu

als je de liefde bedrijft op jullie leeftijd

Ni hatari kwa maisha ya badae

is dat een gevaar voor het leven daarna

6.

Tanzania ya jana siyo ya juzi

Tanzania van gisteren is niet dat van eergisteren

Tanzania ya leo siyo ya jana

Tanzania van vandaag is niet dat van gisteren

Wanafunzi someni muelimike

Leerlingen leer verder zodat jullie ontwikkeld zijn

Ni kesho muendeleze taifa

Morgen moeten jullie het land leiden

Vishawishi na tamaa za kimwili
 Vermijd verleidingen en lichamelijke begeerten
Epukeni ni hatari kwa maisha
 ze zijn een gevaar voor het leven
Mkisema hapana iwe ya kweli
 het zou goed zijn als jullie nee zeggen
Pia mwili ufanane na hapana
 en ook tegen het lichaam nee zeggen

Lied 9

Kampeni ya upimaji afya ‘Campagne testen van gezondheid’

1

Limeshapigwa la mugambo nchini,
 De oproep tot vergadering heeft in het land geklonken
laashiria jambo jema nchini
 een goede zaak vraagt de aandacht in het land
ni kwa ajuza, shaibu na vijana,
 een oproep voor oude vrouwen en mannen en jonge mensen
latualika wote watanzania
 het is een uitnodiging voor alle Tanzanianen
Tujitokeze wote watanzania
 laten alle Tanzanianen verschijnen
Twende kupima afya zetu kwa hiari
 laten we onze gezondheid vrijwillig testen
Ni tendo jema kujua afya zetu
 Het is goed als je weet hoe het met je gezondheid is
Ili tuishi bila hofu na shaka
 zodat je zonder vrees en twijfel kunt leven

2

tuondokane na imani potofu,
 laten we ontrouw afzweren
watanzania tujue tuendako
 Tanzanianen, weet waar we naar op weg zijn
Tunosema kupima kwa hiari,
 wij zeggen jullie: laat je vrijwillig testen
watanzania sikiliza maneno
 Tanzanianen, luister naar deze woorden
Kwenda kupima kwa hiari sikia
 Laat je vrijwillig testen, luister
Ni kuchukua uamuzi mwenyewe
 neem zelf het besluit

Ni wewe baba mama nawe kijana
 jij meneer, mevrouw en jonge man,
Kwenda kupima bila kulazimisha
 laat je testen zonder dat je er toe verplicht wordt

3

Rais wetu Jakaya wa Kikwete,
 Onze president Jakaya Kikwete
kesha fungua njia sasa i-wazi
 heeft een duidelijk voorbeeld gegeven
Kwa hiari yake kuamua kwa dhati,
 vrijwillig heeft hij oprecht besloten
kupima afya pamoja na Mrs
 om zich samen met zijn echtgenote te laten testen
Ondoa shaka na wewe nenda sasa
 twijfel niet langer en ga nu
Rais wetu umuunge mkono
 volg het voorbeeld van onze president
Majibu yako utapewa mwenyewe
 jij alleen krijgt de uitslag van de test
Hiyo ni siri ndani ya siri kali
 de uitslag blijft strikt geheim

4

Wapi tuende tukupate huduma,
 Waar kunnen we terecht voor diensten of zorg
Ya ushauri nasaha na kupima
 voor consultatie, advies en onderzoek
Vituo vipo ni vingi twavitaja,
 er zijn vele plekken die we je hiervoor kunnen adviseren
tega sikio usikie maneno
 luister zorgvuldig
Twende angaza na DDH Bunda
 ga naar het DDH ziekenhuis in Bunda
Twende Huyamu twende CRS
 ga naar Huyamu, ga naar CRS
Twende Kisorija twende kule Ikizu
 ga naar Kisorija, ga ginds naar Ikizu
Huduma safi ya kupima ni tele
 er zijn vele goede zorgvoorzieningen waar je je kunt laten testen

5

Tuondeni hofu na wasiwasi,
 laten we ophouden bang te zijn en zorgen te maken

twendeni sasa nafasi ziko wazi
 laten we nu naar een goede plek gaan
Faida kubwa utakayoipata,
 je zult veel vertrouwen krijgen
ukisha pima afya yako sikia
 als je je gezondheid laat testen, luister
Utatambua hali ya afya yako
 je zult je gezondheidstoestand kennen
Iko salama au ina virusi
 of je gezond bent of besmet bent met het virus
Ukitambua afya yako ni salama
 als je de uitslag krijgt dat je gezond bent
Utajilinda usijiambukizwa
 bescherm dan je zelf zodat je niet besmet raakt
Ukitambua afya yako ina virusi
 als je te horen krijgt dat je besmet bent
Utaishi kwa matumaini sana
 leef dan met veel hoop verder

Lied 10

Kumbukumbu ya mwaka 1983 ‘Herinneringen aan het jaar 1983’

1

Mwaka ule themanini na tatu tuukumbuke
 Laten we het jaar 1983 herdenken
Lilipoingia joka, joka lenye sumu kali
 het jaar waarin de slang, de slang met sterk gif het land binnenkwam
Joka hilo si jingine ni gonjwa sugu Ukimwi
 deze slang is niet anders dan de ernstige ziekte aids
Uliingia nchini mara ya kwanza Kagera
 Voor het eerst kwam de ziekte het land binnen in het Kagera district
Tokea wakati huo ni miaka robo karne
 in de volgende 25 jaar
Joka hilo linazidi kumeza watanzania
 ging de slang door met het verzwelgen van Tanzanianen
Akitokea mmoja ameshanaswa ukimwi
 als je iemand ontmoet die aids heeft
Ujue wapo sitini wale wasijulikana
 weet dan dat er nog zestig meer zijn die je niet bekend zijn

2

Neno ukimwi jamani kirefu chake sikia
 het woord *ukimwi* is lang, luister

Ni upungufu wa kinga mwilini tunakwambia

het is de afkorting van: tekort aan weerstand van het lichaam

Husababishwa na HIV sikiliza

het wordt veroorzaakt door HIV, luister,

Virus vile hatari kwa kudhoofisha afya

dat virus is een gevaar voor de gezondheid

Makao yake makuu virus hivi sikia

dit virus verblijft vooral

Hupatikana mwilini damu na majini ya uke

in het bloed en vagina

Na pia kwenye maziwa ya mama vijazana

en in moedermelk

3

Zipo njia mbalimbali ambazo zasababisha

er zijn verschillende manieren waarop

Kuenea kwa virus baadhi tunatamka

het virus zich verspreidt, we noemen er een paar

Ukimwi unaenea kwa njia ya usherati

aids verspreidt zich door overspel

Pia kushirikiana vifaa vya ncha kali

en ook als we spullen delen zoals scherpe punten

Kutoga pia kuchanja pia na kutaahiriwa

door middel van piercing en snijwonden kun je besmet worden

Kwa kujipanga foleni kunaeneza ukimwi

je kunt zelf makkelijk aids oplopen

Unapongezwa damu bila kupimwa ogopa

als je bloed krijgt dat niet onderzocht is, wees dan beducht

Utavipata virus bila ya kutarajia

dat je het virus kunt oplopen zonder dat je het weet

4

Jamani tujaepuke mazingira ya hatari

Mensen laten we gevaarlijke plekken vermijden

Ambayo yanachangia kuenea kwa ukimwi

waar je makkelijk aids kunt oplopen

Kwenye nyumba za vileo na za kulala wageni

in drankgelegenheden en gasthuizen

Mazingira hatari kwa kuenea ukimwi

gevaarlijke plekken waar je aids kunt oplopen

Palipo na mikutano ya dini hasa usiku

daar waar gebedsdiensten worden gehouden vooral 's nachts

Na kule kwenye viwanda virusi vinaenea
en in industrieën verspreidt het virus zich
Kwenye visiwa na bichi na disco la usiku
op naaktstranden en in disco's 's nachts
Mazingira hayo hatari jamani tuyaepuke
dit zijn gevaarlijke plekken, laten we die vermijden

5

Zipo baadhi ya mila na desturi sikia
Er zijn zeden en gewoonten, luister,
Zinachangia kwa kasi kuenea kwa nyambizi
die de verspreiding van aids bevorderen
Kuoga wazi mitoni ziwani kunachangia
zoals naakt baden in rivier of meer
Kuenea kwa virusi wanawake jiepushe
vrouwen, vermijd
Uvaaji wa vimini na nguo za mipasuo
het dragen van korte rokjes en kleding met een split
Mazoea hayo hatari mabinti mjiushe
deze zaken zijn gevaarlijk, meisjes, vermijd ze
Unapo rithi wajane na kutakasa vilio
het erven weduwen en het reinigen van lijken
Mila hiyo ya zamani imezapitwa wakali
deze gewoonten van vroeger zijn gevaarlijk

6

Jamani tujihadhari tuchukue tahadhari
mensen, laten we voorzichtig zijn, laten we voorzorg nemen
Tuzibue masikio tusikie maarifa
open je oren en luister naar de informatie
Uwe na mwenzi mmoja yule unayemwana
blijf bij een geliefde, die
Aliyeendea kupima afya kwa majibu powa
zich heeft laten testen en een goede uitslag had
Kuweni waadilifu kwenye ndoa wana ndoa
wees trouw in het huwelijk
Msiyooa jamani nendeni kwa tahadhari
en zij die nog niet getrouwd zijn: wees voorzichtig
Atakae puuzia sisi tumeshawaambia
als je de adviezen in de wind slaat, we hebben het al gezegd:
Kila mtu atabeba mzigo wake mwenyewe
iedereen draagt zijn last zelf

Lied 11

Vijana 'Jonge mensen'

1.

Vijana enyi vijana, vijana wenzetu

Jonge mensen, o jonge mensen, onze jeugd

Tumekuwaje vijana, mbona tunachekwa

wat is er met ons gebeurd mensen, waarom wordt er om ons gelachen

Vijana enyi vijana mbona twaumbuka

jeugd, o jeugd, waarom schamen wij ons om jullie

Mbona tunaathirika bila kutambua

waarom zijn wij besmet zonder dat te erkennen

Thamani ya Utu wetu yapotea

de waarde van het leven zijn we kwijt

Pia twakosa heshima katika familia

ook hebben we geen respect meer voor familie

2.

Ujana wetu kijana sisi wa kileo

jeugd, wij jongeren van nu

Uwe wa mafanikio katika familia

laten we ons inzetten voor de familie

Vijana tunatakiwa tuwe waunguana

jeugd, we willen graag dat we samenwerken

Ujana wetu vijana uwe ni wakazi

jeugd, onze jeugd laten we samen inwoners zijn

Huko kwenye kaya sisi tuwe mbele

laten we in de familie voorwaarts gaan

Matendo yetu mazuri yavute wengine

laten onze goede daden aanzetten tot andere

3.

Yapo twaitwa vijana eti wa kisasa

wij spreken jullie aan jeugd van tegenwoordig

Mbona twakosa heshima mbele wa wengine

waarom zien we geen respect van jullie voor anderen

Kuiga kunya kwa tembo ni hatari sana

het is erg gevaarlijk om de manier van poepen van de olifant na te bootsen

Mbona fulani ni chizi wewe unaiga

waarom doe je een vreemd persoon na

Waacheni wafu wazikane wao
 er zijn genoeg overledenen thuis
Hiyo siyo fani yako kijana elewa
 dit is niet wat jullie moeten willen, mensen, begrijp het goed,
Kijana yetu halisi ni huyu sikia
 onze echte jeugd is hij, luister
Tukweleze kijana upate mwangaza
 laten we hem uitleg geven om hem te informeren
Ni yule anayelala akiwaza kazi
 hij die slaapt en aan zijn werk denkt
Kazi halali kwa umma na jamii yake
 echt werk voor samenleving en familie
Ni mtendaji wa kazi za maendeleo
 Hij brengt met zijn werk vooruitgang
Kijana halisi wa si mgomvi
 een echte vent is niet twistziek
Upenda maisha yake yenye afya njema
 hij houdt van het leven in goede gezondheid

4.

Kijana kijana, kijana jilinde
 jeugd, jeugd, jeugd, bescherm jezelf
Hifadhi maisha yako usiyakatishe
 bescherm je leven en breng het niet in gevaar
jilinde kuvuta bangi na pombe kulewa
 bescherm jezelf door geen hash te roken en je te bezatten met
 alcohol
epuka uasherati utaangamia
 vermijd overspel, je gaat er aan onderdoor
kuzurura bila kazi utaitwa mwizi
 als je zonder werk rondhangt word je een dief genoemd
jilinde kijana kuvuta madawa
 vermijd drugs te gebruiken
Ki: kijana we kijana
 jeugd, jij jeugd
Wi: kijana wa kijiji
 jonge mensen in het dorp
Ki: wewe ndio kiongozi
 jij bent echt de leider
K: wa taifa la kesho
 van de toekomstige generatie

K: Onesha tabia njema
 laat goed gedrag zien
K: kwa wakubwa na wadogo
 aan volwassenen en kinderen
K: epuka uasherati
 vermijd overspel
K: usije naswa miwaya
 zodat je geen aids krijgt

Lied 12

Usawa wa wanawake ‘Gelijkwaardigheid van vrouwen
Kweli na haki
 het is een feit en een recht
Ya wanawake
 van vrouwen
Ni kilio cha akina mama
 het is de klacht van iedere vrouw
Wanawake wananyimwa haki
 dat vrouwen rechten onthouden worden
Wanapigwa kama mba mwitu
 ze worden geslagen alsof ze wilde honden zijn
Kweli wanapuuzwa
 echt, ze worden veracht
Ha-ha
 ha,ha
Wanawake na wamechoka wamevumilia sana
 vrouwen zijn het helemaal beu om
unyama wanatendwa na wanaume—wanalaani
 de beestachtigheid van mannen te verdragen- ze vervloeken het
Akina mama
 iedere vrouw
Wanawake walio wengi wanapigwa kama wanyama.
 Vele vrouwen worden geslagen alsof het beesten zijn

Wanatukanwa ovyo jamani, wananyanyaswa,
 ze worden erg beledigd, mensen, ze worden lastig gevallen
wanapuuzwa, wadhalilisha na kunyimwa haki na
 ze worden veracht, ze worden miserabel behandeld, er worden hen
 rechten onthouden, en
wanakatishwa hata tamaa.
 vooral de moed ontnomen

Hivi ni kweli

dit is echt waar

Kama unabisha nenda kwa fulani uone mateso anayopata

als je hier niet mee eens bent, ga dan naar iemand in de buurt en zie hoe de echtgenote en kinderen te lijden hebben,

mke na watoto wa jiraniyo ni sikitiko.

Het is diep triest

Mwanaumme ni waajabu akishapata pesa kidogo

mannen, het is verbazingwekkend, als ze een beetje geld krijgen

Utanona anavinjari na nyumba ndogo

nemen ze een buitenvrouw

Kula kwenyewe

wat betreft het eten daar

Chakula alacho mama mdogo chipsi mayai, nyama ya

de buitenvrouw krijgt frietjes, eieren, kip,

kuku, ugali wa sembe, chai ni soda, utashangaa kwa

puree van mais, frisdrank als ontbijt, je staat er versteld van hoe hij in die tijd de baas speelt

muda huo eti ni bosi tena kibosile aso na shida

maar dit levert ook problemen

Nyumbani kwake

thuis

Nyumbani kwake mama na watoto huambulia dagaa

thuis krijgen moeder en de kinderen alleen maar kleine visjes

peke bila viungu, wakati mwingine wanashindia uji wa udaga ni matatizo

zonder kruiden, op andere momenten is het moeilijk om pap met visjes te krijgen

Mwanamke aseme nini kwa mwanamme

wat moet de vrouw tegen de man zeggen

Akisema ni matatizo makubwa sana

als ze er iets over zegt dan levert dat grote problemen op

Bwana kalewa

de man, dronken

Kurudi kwake ndiyo usiku mwanamke anafokewa

komt 's nachts thuis en de vrouw wordt uitgescholden

fungua mlango awe nyamela akichelewa ndio

als ze te laat de deur opent wordt ze uitgescholden

mateke mwanamke atapigwa sana na kuvunjawa meno

de vrouw krijgt flinke klappen en haar tanden worden gebroken

pia na taraka yapatikana usiku huo.

En deze nacht slapen ze niet bij elkaar

Maulana kaumba dunia jamani
 de Heer schiep de wereld, mensen
kaumba dunia twishi kwa Amani na tupendane
 hij schiep de wereld en laten we in vrede leven en van elkaar houden
enyi, wanaume acheni manyanyaso kwa wanawake.
 O mensen, mannen stop het brute gedrag jegens vrouwen
Dumisheni ndoa mwishi kwa upendo heshima mbele
 Houdt het huwelijk met liefde en respect tot het einde toe in stand
mmeukumbuke mkeo ni Mgomba upalilie
 en denk er aan: je vrouw is de bananenplantage die je moet
 onderhouden

Appendix 3 Utenzi

Utenzi 1

Nyumba ikishika moto, je, tuokoe mali kwanza
 ‘Als het huis vlam vat, laten we dan eerst de bezittingen redden.’

1.

Twasimama mbele yenu, enyi wetu waungwane,
 Wij staan hier voor jullie, die naar ons gekomen zijn
Ujumbe kwa kwenu, wazee pia vijana,
 De boodschap aan jullie, oud en jong is,
Acheni kelele zenu, tuwapeni ya kufanya
 Hou op met jullie lawaai, we zeggen wat jullie moeten doen.

Nyumba imeshika moto, twakoe mali kwanza
 Als het huis vlam vat, laten we eerst de bezittingen redden

2

Nyumba imeshika moto, twakoe mali kwanza,
 Als het huis vlam vat, laten we dan eerst de bezittingen redden

Kina baba na watoto, wa Musoma pia Mwanza
 Alle volwassenen en kinderen van Musoma tot Mwanza

Ukimwi sasa ni moto, kwa kuwa? Ni wa kwanza
 Aids is nu vuur, waarom?

Kujua ulikotoka hiyo siyo dawa yake
 Allereerst, weten waar het vandaan komt levert geen oplossing op

3.

Kujua uliko toka, hiyo iwe ni ziada,
 Weten waar het vandaan komt, heeft geen meerwaarde

Muhimu ni kuepuka, mapenzi kwenye minada
 Het is belangrijk commerciële seks te vermijden

Bara letu Afrika, Ukimwi ni kadakada,

Ons continent Afrika is er zeker aids

Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia

Laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen

4.

Ukimwi yunao sasa, upo hadi kwenye chumba,

We hebben nu aids tot in onze kamer

Wenye mali na mapesa, Ukimwi unawalamba,

Aids likt aan hen die rijkdom en geld hebben

Ukiwaona madensa, hao wako kwenye kamba,

Als je die gekken ziet, ze zitten aan het touw

Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia

Laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen

5.

Ukimwi twaueneza, kwa tabia zetu mbaya,

Aids verspreidt zich bij ons door ons slechte gedrag

Maisha twayapoteza, kwa kununua malaya,

We verliezen het leven door prostituees te bezoeken

Ukimwona Tereza, wanaume mnapwaya,

Als je Teresa ziet, jullie mannen zijn dan verloren

Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia

Laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen

6.

Wengi tunasema kwamba, eti kufa ni kulala

Vele onder ons zeggen dat sterven is als slapen

Mitaani tunatamba, Ukimwi upo Ilala,

Wij verkondigen op straat, dat aids daar slaapt

Siku utapokukumba, utaizima mikwala,

Op de dag dat hij je aanvalt, stopt hij alle regels

Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia

Laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen.

7.

Kung'ang'amia mapenzi, ilikuwa huko nyuma,

Volharden in de liefde, zoals in het verleden

Ni bora uwe na mwenzi, aliyeenda kupima,

Het is beter als je een partner hebt dat hij zich laat testen

Kufanya ovyo mapenzi, mshahara ni kihama,

Als je de vrije liefde bedrijft. Is het resultaat het laatste oordeel

Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia

Laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen

8.

Wanawake epukeni, msiufanye utani,

Vrouwen vermijdt het om duivelse zaken te bedrijven

Ninyi ndio namba wani, asimilia sitini,

Jullie staan echt op nummer 1, met een percentage van 60%

Viungo vyenu laini, kwa kumnasa shetani,

met jullie tedere gewrichten, lokken jullie de duivel in de val

Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia

Laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen

9.

Ukimwi ni janga kwetu, sisi tulio na uhai,

Aids is een ramp bij ons, die nog in leven zijn

Umeshawaua wenzetu, tumbaki majeruhi,

Aids heeft reeds onze geliefden gedood, wij blijven gewond achter

Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia

laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen

10.

Wenye asali limamu, punguani na vichaa,

Zij die lekkere honing hebben, doe niet zo stom

Na wale wendawazimu, Ukimwi wafagilia,

Zij die gek zijn, aids zal hen wegvagen

Unatuua kwa zamu, kaburini twaishia,

Hij zal ons stelselmatig doden, we zullen in het graf leven

Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia

laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen

11.

*Siige kunya kwa tembo, utapasuka msamba,*Poep niet als een olifant, je zult je anus scheuren¹⁸³*Eti uone warembo, unatamani kulamba,*

als je mooie vrouwen ziet en naar hen verlangt

Utanaswa na urimbo, ushindwe kujenga nyumba,

zul je met de stok geslagen worden, het lukt je niet meer een huis te bouwen

Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia

Laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen

12.

Tamati wake watama mbele yenu twaondoka,

Wij zijn aan het einde gekomen en vertrekken

¹⁸³ Swahili spreekwoord: dit spreekwoord is een waarschuwing om niet te imiteren zonder na te denken.

Yote tuliyo yasema, mhimu mkayashika,
 We hebben jullie alles al gezegd, het is belangrijk dat jullie het
 begrijpen
Kina baba kina mama, dada pia kina kaka
 Mannen, vrouwen, zusjes en broertjes
Tuepukeni Ukimwi, kwa kubadili tabia
 laten we aids vermijden door ons gedrag te veranderen

Utenzi 2

1. *Hakika imenipasa kunena yalo moyoni*
 Het is zeker nodig om tot jullie hart te spreken
Umetusibu mkasa, Ukimwi ulimwenguni
 Er is bij ons iets gebeurd, aids is in de wereld
Ni maradhi ya kisasa, tiba haipatikani,
 Het is een ziekte van nu, behandeling er voor is er niet
Ukimwi ni pigo zito, jamani tujihadhari
 Aids is een grote schok, mensen laten we oplettend zijn.
2. *Chanzo chake ni zinaa, na shindano za magendo*
 De ziekte begint met geslachtsziekte en met naalden van de zwarte
 markt
Kujiepusha yafaa, kubadilisha mwenendo
 Het is goed om de ziekte te vermijden door je gedrag te veranderen
Ukimwi kweli waua, ni kheri kufa kwa sondo
 Aids doodt jullie echt, het is als sterven door houtworm
Vijana pia watoto, Ukimwi wafagilia.
 Jongeren en kinderen, aids zal hen wegvagen
3. *Tiba haipatikani, mabingwa wamesaini,*
 Behandeling is er niet, geleerden bevestigen dat
Kutangaza redioni, na pia magazetini,
 Op radio en in kranten wordt verkondigd
Dunia-i mashakani, kwa pigo hili haini,
 Dat de wereld vertwijfeld is, door deze schok,
Hakuna njia ya mkato, dawa ni kuacha ngono.
 Er bestaat geen korte route, het geneesmiddel is om onveilige seks te
 vermijden.
4. *Acheni migogoro, sogea tuelezane*
 Laat de conflicten achterweg, laten we elkaar uitleggen
Anzishevu kwanza kongamano, ukweli tuambizane,
 We hebben de bijeenkomst georganiseerd, laten we de waarheid
 spreken

Juu ya haya maono, heri tuelimishane

Wat betreft deze meningen, is het beter elkaar uit te leggen

Tuweze kuzima moto, sisi tulio hai bado

Dat we in staat zijn het vuur te doven, zolang we nog in leven zijn.

5. *Uwe na mwenzi mmoja, aliyejaa heshima,*

Houd het bij één geliefde, vol met respect

Muungane kwa pamoja, afyaze mwende kupima

Ga samen je gezondheid laten onderzoeken,

Usilamani mapaja, nyambizi utakuuma,

Verlang niet naar slechte zaken, aids zal je pijn doen

Utayapata majuto, punde utakapolazwa.

Als je er spijt over krijgt, zul je spoedig opgenomen worden

6. *Wasichana epukeni, kuvamia wapitao*

Jonge meiden, vermijd voorbijgangers aan te vallen

Uwezi ukabaini, ni yupe asiye nao

Je kunt niet zien, wie het niet heeft

Kwa pesa msitamani, msije mkwawe nao

Verlang niet naar geld dat je niet hebt

Pitieni njia fupi, kwa ndoa mkaolewe

Kies voor de korte weg, voor het huwelijk, ga trouwen.

7. *Ukishanaswa shetani, kwa kutambua dalili,*

Als je al door de duivel bent gepakt en symptomen herkent

Vema, uwe hadharani, uwahi hospitali

Goed, maak het kenbaar en ga naar het ziekenhuis

Usijabu asilani, kwa mapenzi ya kimwili

Antwoord niet met persoonlijke liefde

Dawa ya moto ni moto, jamani tujielewe

Bestrijd vuur met vuur, mensen begrijp dat.

8. *Jamani tuwe na upendo, kwa wake wagonjwa wetu*

Mensen laten we liefdevol zijn voor de zieken onder ons

Tuwalee kwa upendo, rafiki na ndugu zetu

Laten we met liefde opvoeden, onze vrienden en naasten

Tusiwafungie fundo, hao bado ni wenzetu

Laten we het contact niet met hen verbreken, het zijn nog steeds de onzen

Tusije kuwatenga, wasije kufa haraka

Laten we ze niet isoleren, zodat ze niet snel sterven.

9. *Shida haina adabu, leo kwako kesho kwangu*

Problemen vertonen geen goed gedrag, vandaag ben jij aan de beurt morgen ik

Gonjwa limeshawasibu, wenzetu kina murungu

De epidemie heeft de onzen al getroffen, het is al een groep

Tuwapeni matibabu, chakula pia dengu

Laten we ze behandelen met voedsel en linzen

Tuwape huduma safi, kama wagonjwa wengine.

Laten we goed voor ze zorgen, zoals we voor andere zieken zorgen.

10. *Hayo tuliyo yasema, bila shaka yatafaa*

We hebben nu deze zaken besproken, zonder twijfel was dat nodig

Hapa sasa tunakwama, kwani imekisha saa

Nu zitten we hier vast omdat de tijd voorbij is

Tusifanye kama Tome, dunia kweli acha

Laten we niet handelen zoals Tome die al overleden is

Mwenye akili limamu, utabadili tabia.

Als je een gezond verstand heb, verander dan je gedrag.

Utenzi 3

Wanafunzi

1

E wanafunzi sikia, mbona mnatupa tabu,

he, leerlingen luister, waarom veroorzaken jullie ellende

Mbona sasa mwapitia, maajuza na mababu,

waarom negeren jullie nu oude mannen en vrouwen

Hakika tunachukia, tutawaapeni adhabu,

wij keuren dat zeker af, wij zullen jullie straffen

Acheni majaribio, mtapasuka misamba

hou op met jullie experimenten, jullie zullen je schaambeen breken

2

Acheni majaribio, mtapasuka misamba,

hou op met jullie experimenten, jullie zullen je schaambeen breken

Mwisho wake ni kilio, shida kwa kina mjomba,

het eindigt in gehuil, problemen met iedere vriend

Yaoneni matukio, kwa wanaotoa mimba,

kijk wat er gebeurt als je zwanger wordt

Acheni majaribio, mtapasuka misamba

hou op met jullie experimenten, jullie zullen je schaambeen breken

3

Juzi tulishuhudia, kwa mwanafunzi mmoja,

Onlangs hebben we wat meegemaakt met een leerling

Pale Kibara sikia, vilikuwa ni viroja,

Daar in Kibara gebeuren vreemde zaken

Shimo tulimchimbia, mauti akayaonja
 we hebben een graf voor haar gegraven, ze is overleden
Alipoitoa mimba, mauti yakamfika
 toen ze abortus had laten plegen is ze er aan overleden
Hasa wewe Athumani, pia na wewe Nyakwesi,
 vooral jij Athumani, en ook jij Nyakwesi
Nyinyi ndio namba wani, mmeshaanza mapenzi,
 ja jullie vooral, jullie zijn al de liefde gaan bedrijven
Mwatembea na wahuni, kwa kutamani mavazi,
 jullie gaan om met lanterfanter
Alipoitoa mimba, mauti yakamfika
 toen ze abortus had laten plegen is ze er aan overleden

5

Mkichezea viungo, vya uzazi wanafunzi,
 als jullie met jullie geslachtsorganen spelen
Mtakatika maungo, mlie kama feruzi,
 krijgen jullie last van gewrichten, jullie zullen huilen als Ferouz¹⁸⁴
Mtapamika migongo, Ukimwi ni kama kazi,
 jullie zullen instorten, aids gaat te werk
Acheni majaribio, mtapasuka misamba.
 hou op met jullie experimenten, jullie zullen je schaambeen breken

6

Enyi mliobalehe, na mliyo na matiti,
 o jullie pubers en zij die al borsten hebben
Msione starehe, kutembea na mabinti,
 ga niet voor de pleziertjes, en voor seks met meisjes
Msipende starehe, msijepatwa mauti,
 als je niet voor de pleziertjes gaat, zul je niet sterven
Acheni majaribio, mtapasuka misamba.
 hou op met jullie experimenten, jullie zullen je schaambeen breken

7

Mimba wakisha watunga, jeuri hamna tena,
 als jullie zwanger zijn, er is geen grotere onbeschaamdheid
Mnaenda kwa wakunga, na madawa mwatafuna,
 dan gaan jullie naar de verloskundige en gebruiken medicijnen
Shida zikisha watinga, mnabaki kulumbana
 als er volop problemen zijn, blijven jullie beargumenteren

¹⁸⁴ Hier wordt verwezen naar de rapper Ferouz, die in zijn lied *Starehe* huilt van spijt dat hij door zijn gedrag aids opgelopen heeft.

Maji yakizidi unga,¹⁸⁵ *matokeo ni majuto*
als water het meel doet toenemen, is het resultaat dat jullie spijt
krijgen

8

Tunaomba mtulie, wadogo zetu walembo
Wij vragen jullie gedraag je netjes¹⁸⁶, zorg voor onze broertjes en
zusjes

Masomo mhudhurie, mjifunze na kimombo,
volg jullie lessen

Ushairi msikie, msome mfike ng'ambo,
luister naar advies, leer zodat je naar het buitenland kunt gaan

Acheni majaribio, mtapasuka misamba
hou op met jullie experimenten, jullie zullen je schaambeen breken

9

Mkawambie wakunga, sheria sasa iwazi,
vertel de verloskundigen, de wet is er tegenwoordig duidelijk in

Watakuja kuwafunga, kuuwa kipyaa kizazi,
dat ze opgesloten zullen worden, voor het doden van nieuw leven

Sheria itawanyonga, heri wapike andazi
de wet maakt een einde aan ze, succes met broodjes bakken

Mnawatoa mimba, wanafunzi mtafungwa
Jullie onderbreken je zwangerschap, leerlingen jullie zullen
gevangen worden gezet

10

Siyo kwamba tumechoka, twapumzisha ubongo,
het is niet omdat we nu vermoeid zijn, maar we laten jullie nu even
nadenken

Marajani Tunatoka, tulosema si uhongo,
Mensen we vertrekken, wat wij gezegd hebben is niet om jullie te
chanteren

Na kama mkiyashika, na kuishi kama konga,
en als jullie het al begrepen hebben en wijs leeft

Wanafunzi mashuleni, mtathaminiwa sana
zullen jullie leerlingen zeer geprezen worden

¹⁸⁵ De uitdrukking *maji yakizidi unga* betekent 'als zaken kapot gaan' (Wamitila 2006)

¹⁸⁶ Letterlijk: wees stil, hou je rustig

Utenzi 4

Ukimwi saizi yenu kama mkitamani pesa

Aids wordt voor jullie een groot probleem als jullie naar geld verlangen

1.

Wadogo zetu wapenzi, usia tunawapeni,

Lieve broertjes en zusjes, we geven jullie raad

Hakika siku za mwizi, ni zile arobaini,

Ongetwijfeld worden de dagen ontnomen, die veertig

Ninyi bado wanafunzi, mapenzi yaepukeni,

Jullie zijn nog leerlingen, vermijd de liefde

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is iets voor later

2.

Someni mwelimike, mliokoe taifa,

Studeer, zorg voor opleiding, zodat je de natie redt

Someni muhesimike, kikata na kitarafa,

Leer, heb respect, in district en regio

Wala msibabaike, na mapenzi ya maafa,

Scharrel niet en bedrijf geen commerciële seks

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is iets voor later

3.

Mapenzi yaepukeni, wanafunzi mashuleni,

Vermijd de liefde, leerlingen

Adui yupo shetani, yupo hadi ofisini,

De vijand is satan, hij komt tot in het kantoor

Mungu sio athumani, twendeni makanisani,

God wordt niet gewaardeerd, laten we naar de kerk gaan

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is voor later

4

Mapenzi mkiyafanya, mngali bado wadogo,

Als jullie de liefde bedrijven terwijl jullie nog jong zijn

Magonjwa mtayasanya, ya zinaa si kidogo,

zullen jullie veel ziekten krijgen, Geslachtsziekten zijn geen kleinigheid

Hapa leo twawakanya, msije pata kisago,

We verbieden jullie het nu vandaag, zodat jullie geen problemen krijgen

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is iets voor later

5

Mapenzi umri wenu, madhara yake ni mingi,

De liefde op jullie leeftijd geeft veel problemen

Utafukuzwa makwenu, kama mkipenda rangi,

Je zult weggestuurd worden uit jullie omgeving, als jullie van kleur houden

Ukimwi saizi yenu, mkitamani shilingi,

Aids is voor jullie een probleem als jullie naar geld verlangen

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is voor later

6

Mtapatwa na zinaa, mkiyafanya mapenzi,

Jullie zullen geslachtsziekten krijgen als jullie de liefde bedrijven

Mtashindwa na kuzaa, kisonono kama kzi,

Jullie zullen geen kinderen op de wereld kunnen zetten, gonorroë doet zijn werk

Ushairi wa kufaa, twawapeni wanafunzi,

We zullen jullie een goed advies geven, leerlingen

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is iets voor later

7

Viungo vyenu vidogo, havumili vishindo,

Jullie gewrichten zijn nog kwetsbaar, ze kunnen nog niet tegen een stootje

Njia zenu bado ndogo, zimezibwa na utando,

Jullie vagina is nog smal en afgesloten door een vliesje

Msichukue vigogo, mitaani kwa mawindo,

Neem geen sukkels, de straten zijn vol met jagers

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is voor later

8

Akili yenu nyembamba, haijui methali,

Jullie verstand is nog beperkt, jullie kennen het spreekwoord niet

Mimba wakisha wamimba, mtalaumu magwali?

Zij die meer dan een keer zwanger zijn, wie geef je dan de schuld?

Yapo kuwa mwajigamba, eti nyie mashuleni,

Als je dus trots wilt zijn op jezelf, ga dan naar school

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is voor later

9

Msimuige fulani, kwa kuona anafanya,

Volg niet het voorbeeld van anderen als je ziet wat ze doen

Yeye huyo ni mhuni, ni virusi mutawanya,

Ze bedrijven prostitutie, verspreiden het virus

Mlioanza acheni, Ukimwi utawanyonya,

Als je het al gedaan hebt: stop er mee, aids zal jullie verstikken

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is voor later

10

Tumefika ukingoni, tulosema yashikeni

We zijn aan het einde gekomen, overdenk wat we gezegd hebben

Msifikiri utani, mkayaweka kapuni,

Denk niet dat het een grap is, neem deze woorden mee

Muhimu muwe makini, elimu iwe kichwani,

Het is belangrijk oplettend te zijn, gebruik je verstand

Someni mwelimike, mapenzi yawe baadae

Studeer, zorg voor opleiding, de liefde is voor later

Appendix 4 Shairi

Shairi 1

UKIMWI sasa tishio ‘Aids is nu een bedreiging’

1.

Nalifungua pazia, ninalo jambo moyoni,

Ik opende de gordijnen, ik heb iets op mijn hart

Ujumbe kuwafikia, utulivu naombeni,

ik breng jullie een boodschap, ik vraag om stilte

Dunia yawakalia, naeleza adhalani,

de wereld huult, ik zal jullie uitleggen waarom

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

ik verklap jullie geen geheim: aids is nu een bedreiging

2.

Ukimwi sasa tishio, dunia yetu vitani

Aids is nu een bedreiging, onze wereld is in oorlog

Ukimwi ni kianzio, vijana twapotezeni

Aids is een startpunt, we verliezen veel jonge mensen

Kila pande ni vilio, si Ulaya si kusini,

Overal klinken rouwliederen, niet in Europa, niet in het zuiden

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

Ik verklap jullie geen geheim: aids is nu een bedreiging

3.

Bwana Ukimwi hatari, akiingia nyumbani,

Meneer, Aids is een gevaar als hij je huis binnen komt

Hapokei ushauri, yeye ngumi mkononi,

hij accepteert geen advies, hij geeft een vuistslag

Njia yake ni ya siri, makao yake mwilini

zijn route is geheim, hij woont in het lichaam

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

ik verklap jullie geen geheim: aids is nu een bedreiging

4.

Penzi lisilo salama, chanzo Ukimwi jueni,

Weet dat onveilig seks het begin van aids is

Enyi baba pia mama, penzi olela hacheni,

o, man en vrouw, laat rampzalige seks achterwege

Viziwi pia vilema, mapenzi yaogopeni,

Doven en gehandicapten, vrees de liefde

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

ik verklap jullie geen geheim: aids is nu een bedreiging

5.

Ulafi wenu wa chini, kasi mpya punguzeni,

Begeerte beneden, verminder jullie nieuwe vaart

Dunia iko mbioni, siyo kama ya zamani,

de wereld is snel, het is niet zoals vroeger

Na denda mlikoneni, chomolea ziacheni,

en orale seks, snelle prostitutie, laat het achterwege

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

ik verklap jullie geen geheim: aids is nu een bedreiging

6.

Wazee mnatisheni, kwa mapenzi namba wani,

oude mannen, jullie zijn een bedreiging nummer een met jullie liefde

Vibinti mwavipendeni, mwasema viko makini,

jullie houden van jonge meiden, jullie geven hen veel aandacht

Aibu mwaondoeni, pesa mwavimwagieni

jullie hebben geen schaamte meer, jullie strooien met geld

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

Ik verklap geen geheim: aids is nu een bedreiging

7.

Vikongwe akina mama, kundi moja hatarini,

oudere vrouwen, iedere vrouw, als een groep zijn jullie in gevaar

Vijana kweni, ni nyama, damu zao ni makini,
 jullie kinderen zijn voedsel en bloed heeft aandacht nodig
Umesahau kihama, umalaya kufanyeni,
 jullie vergaten te verhuizen, prostitués werden bezocht
Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio
 ik verklap geen geheim: aids is nu een bedreiging

8.

Enyi mama wenye nyumba, manakasi eleweni,
 O huisvrouw, begrijp goed,
Hamjali zenu nyumba, Uloho mwaugaweni
 jullie letten niet goed op jullie huis, begeerte brengt schade
Ndoa zetu ni kuyumba, Ukimwi mwauleteni,
 ons huwelijk is aan het wankelen, jullie hebben aids gebracht
Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio
 ik verklap geen geheim: aids is nu een bedreiging

9.

Ukeketaji hacheni, Ukimwi angamizeni,
 Laat tatoeages achterwege, aids werkt vernietigend
Sindano za mitaani, ni ukoma ogopeni,
 spuiten gevonden op straat, kun je vrezen als lepra
Ngono nzembe tuacheni, Ukimwi kuepukeni,
 laat casual seks achterwege, vermijdt aids
Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio
 ik verklap geen geheim: aids is nu een bedreiging

10.

Mabingwa madaktari, dawa zimewakoseni,
 geleerde dokters, ze hebben geen medicijnen
Wamebaki washauri, Ukimwi kujikingeni
 wat nog rest is advies, bescherm je tegen aids
Punguzeni Ujeuri, msije angamieni,
 laten we de ongemanierdheid verminderen, vorm geen bedreiging
Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio
 ik verklap geen geheim: aids is nu een bedreiging

11.

Na magonjwa ya zinaa, nayo myafahamuni,
 en geslachtsziekte, jullie kennen die al
Kaswende ikikomaa, hatari kubwa mwilini
 syfilis als het erger wordt, is een groot gevaar voor het lichaam
Kisonono chatambaa, kona zote za uhuni
 gonorroe verspreidt zich, overal waar prostitutie is

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

ik verklap geen geheim: aids is nu een bedreiging

12.

Utasa pia ugumba, ni zinaa sikieni

Steriliteit en infertiliteit, heeft te maken met overspel luister,

Siku zote uwakumba, ngono kuinezeeni,

jullie krijgen er mee te maken als jullie met onveilige seks doorgaan

Wenye penzi la kuyumba, ni hatari maishani,

onveilige seks vormt een gevaar voor het leven

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

ik verklap geen geheim: aids is nu een bedreiging

13.

Ushauri natoeni, vema kuufuateni,

ik geef nu advies, volg het goed op

Kondomu mtumeieni, Ukimwi mjikingeni,

gebruik een condoom, zo bescherm je jezelf tegen aids

Mpenzi machagueni, mmoja mwenye imani,

kies je geliefde, één trouwe geliefde

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

ik verklap geen geheim: aids is nu een bedreiging

14.

Nafunga langu pazia, naenda kwetu nyumbani,

ik sluit mijn gordijnen, ik ga naar huis

Mitaani naishi, neno nimelitoeni

ik woon in de buurt, ik heb gesproken

Mungu Baba kasikia, kaniweka mikononi,

God luister, ik geef me aan u over

Natoboa siyo siri, Ukimwi sasa tishio

ik verklap geen geheim, aids is nu een bedreiging

Shairi 2

Wasia Tubadilike tuepe UKIMWI 'Waarschuwing dat we moeten veranderen om aids te vermijden'

1.

Naja kwenu kuhubiri, uwanjani naingia

Ik ben naar jullie gekomen om te preken, ik betreed het podium¹⁸⁷

Nikiwa nayo mazuri, yote nitasimulia,

Als ik iets moois had, zou ik het allemaal vertellen

¹⁸⁷ *Uwanja* betekent 'open ruimte', hiermee wordt bedoeld de open ruimte in het dorp waar de performance gehouden wordt

Litakuwa jambo zuri, wote tukizingatia,

Het zou prachtig zijn als wij allemaal hierover na willen denken

Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi

Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

2.

Hakika tujihadhari, Ukimwi watumaliza

Laten we echt voorzichtig zijn, aids richt ons te gronde

Kwani ni gonjwa hatari, kwa wingi

Want het is een gevaarlijke ziekte, die velen van

linatumeza

ons opgeslokt heeft,

Tusipo kuwa hodari, maisha tutapoteza,

Als we dit niet serieus aanpakken, zullen we het leven verliezen

Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi

Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

3.

Tunda lilikuwa tamu, kwa sasa linauuozo,

De vrucht was lekker, maar is nu verrot

Yabidi tuwe timamu, kuvumilia ndo wazo,

Laten we verstandig zijn, en er aan blijven denken

Hatutaishiwa damu, akili tukiwa nazo,

Als we geen bloed meer hebben, hebben we nog verstand

Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi

Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

4.

Jambo ninalowaomba, kila mke atambue,

Wat we jullie vragen, ieder vrouw zal dat erkennen

Tuache kulambalamba, ua, zuri tuchague,

Laten we overspel achterwege laten, een bloem, laten we een mooie kiezen

Maisha tutayachimba, uzinzi tuubague,

Het leven heeft ons al veel problemen bezorgd, laten we overspel achterwege laten

Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi

Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

5.

Vijana wengi usema, Ukimwi ni radioni,

Jongeren er wordt veel gesproken Aids is op de radio

Hili siyo jambo jema, bali ni lenye huzuni,

Het gaat niet over iets moois, maar over iets verdrietigs

Ukimwi unawauma, wasio jali maoni,
Aids doodt jullie, als jullie niet goed nadenken
Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi
Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

6.

Vijana sisi ndo nguzo, yafaa tuwe imara,
Jongeren, wij zijn inderdaad de steunpilaren, het past ons sterk te zijn
Tusiwe wenye miozo, kuugua kila mara,
Als we niet oplettend zijn, bezeren we ons iedere keer
Tukiufanya mchezo, tutakumbua na madhara,
Als we blijven spelen, zullen we ziekten oplopen
Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi
Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

7.

Taifa bila vijana, na siyo taifa tena,
Een samenleving zonder jongeren, is geen samenleving meer
Kwa kazi tukiungana, matunda utayaona,
Als we ons verenigen om de klus samen te klaren, zullen we de vruchten er van plukken
IDD lilimtafuna, alipoleta ubwana,
IDD kauwt, en bracht overheersing
Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi
Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

8.

Napenda kuwaambia, nyie dada ndo sababu,
Ik wil jullie zeggen, jullie zusters, ja er is een oorzaak
Acheni mbaya tabia, kuweni wastarabu,
Laat jullie slecht gedrag achterwege, wees beschaafd
Mwashindwa kujizuia, kwa mtindo ya ajabu,
Jullie zijn er niet in geslaagd de controle over jullie zelf te hebben, op een verbazingwekkende manier
Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi
Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

9.

Ndo ninyi mnachochea, Ukimwi kuongezeka,
Het is zeker dat als jullie doorgaan met jullie spelletjes, aids zal toenemen
Mtindo mmependea, ya Ulaya Amerika,
Jullie houden van de Europese, Amerikaans stijl

Kwa mavazi na tembea, waume wanachemka,

Met jullie kleding en manier van lopen, winden jullie mannen op

Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi

Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

10.

Hata muwe vilioni, mwavaa vyenu vimini,

Jullie zijn zelfs met miljarden, en dragen korte rokjes

Pengine hata hodini, aibu hamuioni,

Soms zelfs in de ochtend, schaamte kennen jullie niet

Hatari sasa njiani, mwayafanya ya kiuni,

Jullie zijn nu een gevaar op de weg, de dingen die jullie doen
zijn van essentieel belang

Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi

Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids
vermijden

11.

Wazee msije moto, wenye busara kuweni,

Oudere mannen, wees niet opgewonden, wees wijs

Mambo yote ni mpito, hamtarudi tumboni,

Alles gaat voorbij, jullie zullen niet in de buik terugkeren

Ridhiken na mapato, ya wake zenu nyumbani,

wees tevreden met wat je thuis hebt

Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi

Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

12.

Watoto mwawadubuni, kwa vihela vya barafu,

Jullie maken kinderen gek met muntstukjes

Mwawafundisha uhuni, kwa matendo ya uchafu

jullie leren hen prostitutie, door vuile handelingen

Mawazo mema toeni, mbeleni tutawasifu

Uit goede gedachten, dan zullen we jullie voortaan prijzen

Mwenendo tuubadili, tuepe gonjwa Ukimwi

Laten we ons gedrag veranderen, zodat we de ziekte aids vermijden

13.

Nisije nikawachosha, hapa tamati nafika,

Laat ik jullie niet verder vermoeien, ik ga eindigen

Mwenendo tuonyeshe, hili gonjwa kuepuka,

vertoon gedrag om deze ziekte te vermijden

Uzinzi usiwe lishe, acha usije anguka,

stop overspel, stop om niet te vallen

Yule mwenye masikio, asikie neno lile
Moge hij die oren heeft, deze woorden gehoord hebben

Shairi 3

Ukimwi, madawa ya kulevya ‘Aids, drugs’

1.

Usingizi nazinduka, ninalo niloliota,
Ik ben plotseling wakker geschrokken, ik had een droom
Limenipa kuteseka, usingizi kutopata,
hij greep me aan, ik kon niet meer slapen
Ni vema kulitamka, lisije leta utata,
Het is goed dat ik hierover vertel, zodat er geen ellende komt
Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.
*Nyambizi*¹⁸⁸ onze vijand vernietigt ons, mensen

2.

Nyambizi atumaliza, ni vema tujielewe,
Nyambizi vernietigt ons, het is goed dat te beseffen
Hawezi hata kusaza, tusipofunga kibwewe,
Niets blijft er over, als wij niet de buikriem aanhalen
Umalaya tukikuza, tutaendeleza yowe,
Als we doorgaan met prostitutie, zullen we blijven schreeuwen om
hulp
Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.
Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

3

Jambo linalowatesa, mie nimeshagundua
Dat wat kwelt heb ik al ontdekt
Matako wakitikisa, wanaume mnatua,
als jullie met de billen schudden, zijn de mannen stil
Mtayamwaga mapesa, Ukimwi mkinunua,
jullie strooien met geld, jullie kopen aids
Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.
Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

4.

Peku peku mwatumia, bila kujali salama,
Jullie bedrijven onbeschermd seks¹⁸⁹, zonder je om veiligheid te
bekommeren

¹⁸⁸ Metaforische benaming voor aids. Zie hoofdstuk 4

¹⁸⁹ *pekupeku* betekent in SS ‘blootvoets’, maar in LyM betekent het ‘onbeschermd seks’

*Ushauri mwaachia, mwajisukuma kwa nyama*¹⁹⁰

Goede raad slaan jullie in de wind, jullie bedrijven graag seks zonder condoom

*Na denda*¹⁹¹ *mwaitikia, mwatupa mbali kiama*

en jullie stemmen in met de Franse zoen, jullie ontkennen het einde van het leven

Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani

Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

5.

Wazee nyie hatari, mwashindana na vijana,

Oudere mannen, jullie zijn een gevaar, jullie wedijveren met jonge kerels

Mwazipepeta habari, mwaibueni vimwana,

Er gaan vele verhalen over jullie, jullie stelen de jonge meiden

Vimwana wa Sekondari, hakika mwavitafuna

de meisjes van de middelbare school, jazekeer jullie verslinden ze

Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.

Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

6.

Vijana mwapumbanika, pigo moja halifai,

Jonge mannen jullie roepen verbazing op, een klap is niet genoeg

Mkono ukishafike, mitaani mwajidai,

masturbatie, opscheppen op straat

Mwekuwa ni vibake, wasio jali uhai,

wat resteert is dat jullie geen zorg dragen voor het leven

Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.

Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

7.

Watu wengi mwabweteka, mwashindwa afya kujua

jullie doen vele mensen naar adem snakken van verbazing, Jullie slagen er niet in jullie gezondheidstoestand te kennen

Mwabaki kunyanyasika, virus kutotambua

Hij die het virus niet erkent zal getergd worden

Mabega yakiinuka, ni vilio mwaangua,

de schouders steken uit, jullie barsten in gejammer uit

Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.

Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

8.

¹⁹⁰ De volledige uitdrukking is *nyama kwa nyama* en betekent 'vlees op vlees'

¹⁹¹ LyM (Reuster-Jahn & Kiessling, 2006)

Upimaji wa hiari, tayari umetolewa,
laat je vrijwillig testen, die boodschap is al gebracht
Rais na mawaziri, ni wa kwanza kutangazwa,
de president en zijn ministers, dat is als eerste vermeldingswaard
Nasi sote tuhiari, twendeni wote kupimwa,
en laten wij allen ons vrijwillig testen
Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.
Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

9.

Aibu pia uwoga, naomba tuondoeni,
Schaamte en angst, ik vraag jullie laten we dat achter ons laten
Nambizi ukishagonga, CRS fiken,
als je al aids hebt opgelopen, ga naar CRS¹⁹²
Mtapata kujipanga, maisha yalefukeni
maak met hen een plan om je leven te verlengen
Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.
Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

10.

Wanawake wasichana, tamaa ipunguzeni,
Vrouwen en meisjes, wees minder wanhopig
Wazee pia vijana, zipu zenu zifungeni,
Oudere en jonge mannen, sluit jullie gulp
Pamoja tukiungana, nyambizi tutang'oeni,
en als we ons ook nog verenigen, kunnen we aids beëindigen
Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani
Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

11.

Iwe siraha kondomu, tendo ngono mkifanya,
laat het wapen het condoom zijn, als jullie seks bedrijven
Demu mmoja muhimu, hasiye kuwa malaya,
dan is het belangrijk om één geliefde te hebben, en niet een prostitué
Penzi liwe la kudumu, na mpeane kwa mwanja,
laat de liefde permanent zijn, en blijf lange tijd bij elkaar
Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.
Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

12.

Si kosa kutamatika, ninakwenda kanisani,
Mijn verhaal is nog niet ten einde, ik ga naar de kerk

¹⁹² CRS is een NGO die steun geeft aan aidspatiënten

Maombi kwake Rabuka (Mungu), kwa pamoja tuombeni,
 daar bid ik tot God, en laten we allen bidden
Ajaze zake baraka, tuweze neemeken,
 dat hij ons geluk geeft, zodat we gezegend zijn
Nyambizi kwetu adui atumaliza jamani.
 Nyambizi onze vijand vernietigt ons, mensen

Shairi 4

Utoaji mimba ‘Zwangerschapsonderbreking’

1.

Ukimiya naondoa, aibu kando naweka
 Ik verbreek het stilzwijgen, de schaamte voorbij
Macho mnayokodoa, nyuma siwezi geuka,
 jullie zetten grote ogen op, ik kan niet terug
Sikuja paka madoa, nanuia kutamka,
 ik kom niet om met modder te gooien, ik kom verkondigen
Wanafunzi namba one, kwa utoaji wa mimba
 leerlingen, jullie staan nummer een wat betreft
 zwangerschapsonderbreking

2.

Kwa utoaji wa mimba, wanafunzi namba wani,
 wat betreft zwangerschapsonderbreking, zijn jullie nummer één
Wanaume mwawabeba, umri bila jalini,
 jullie gaan om met mannen, zonder op hun leeftijd te letten
Mwajifanya mnaiba, tokeo mwaibikeni,
 jullie bestellen je zelf, met als resultaat dat jullie berooid achter
 blijven
Wanafunzi namba one, kwa utoaji wa mimba
 leerlingen jullie staan nummer een wat betreft
 zwangerschapsonderbreking

3.

Enyi mnatutisheni, kona zote za dunia,
 O, jullie jagen ons schrik aan, overal ter wereld,
Kwa ngono mkomakini, kitabu mnaachia,
 door je zo op seks te richten, de boeken hebben jullie verlaten
Hesima mnaondoeni, babu kaka mwapitia,
 respect is er niet meer, opa, broers, laten jullie links liggen
Wanafunzi namba one, kwa utoaji wa mimba
 leerlingen jullie staan nummer een wat betreft
 zwangerschapsonderbreking

4.

Hakika ninyi mabinti, uhuni mwaukalia,
Zeker, jullie meiden, houden je bezig met prostitutie
Hamkai kwenye kiti, dunia mwapalamia,
jullie zitten niet stil, jullie struinen de wereld rond
Muotapo viona titi, mapenzi mwakimbilia,
zodra jullie borsten krijgen, zoeken jullie toevlucht bij de liefde
Wanafunzi namba one, kwa utoaju wa mimba
leerlingen jullie staan nummer een wat betreft
zwangerschapsonderbreking

5.

Mimba wakishawapiga, hamnao uthamani,
Als jullie al zwanger zijn kennen jullie geen normen
Mayowe mtayabwaya, bwana zenu vizingani,
jullie hebben de pleidooien genegeerd, jullie draaien om de mannen
heen
Na mtindo mlo iga, kwa mimba ni mfukoni
jullie bootsen de moderne mode na, zwanger en wel
Wanafunzi namba one, kwa utoaju wa mimba
leerlingen jullie staan nummer een wat betreft zwangerschaps-
onderbreking

6.

Dawa mgundueni, ni mimba kuzitoeni,
jullie hebben medicijnen ontdekt om de zwangerschap te
onderbreken
Viumbe mwavivueni, mauti mwatafuteni,
jullie doden de embryo's, jullie hebben de lijkes verstopt
Jera miaka therathini, sheria yetu nchini
dertig jaar gevangenisstraf staat er op volgens de wetten in ons land
Wanafunzi namba one, kwa utoaju wa mimba
leerlingen jullie staan nummer een wat betreft zwangerschaps-
onderbreking

7.

Chooni mwawatupeni, kentozi ni masanduku,
Jullie gooien ze in het toilet, in plastic zakken
Jalala vichuguuni, ni makaburi lukuku,
jullie dumpen ze in termietennesten, graven in overvloed
Mazishi mwiko jioni, yenu mwafanya usiku,
jullie begraven 's avonds, als het donker is
Wanafunzi namba one, kwa utoaju wa mimba
leerlingen jullie staan nummer een wat betreft zwangerschaps-
onderbreking

8.

Wavuvi mwakimbilia, eti wanyo mapesa,
 jullie draaien om de vissers heen, want zij hebben geld
Magonjwa wawaachia, mwakalibisha utasa,
 jullie veronachtzamen ziekten, jullie verwelkomen onvruchtbaarheid
Ukimwi wawajaria, mwajitwika kwa anasa,
 jullie bezorgen anderen aids, jullie zoeken pleziertjes in jullie leven
Wanafunzi namba one, kwa utoaju wa mimba
 leerlingen jullie staan nummer een wat betreft zwangerschaps-
 onderbreking

9.

Na wakiume vijana, mwatisheni kwa mahaba,
 en jullie jonge mannen, jullie vormen een bedreiging met jullie
 liefde
Mwawasaka wasichana, kwa pia umimba
 jullie jagen op jonge meiden en maken ze zwanger
Mwawatafuna, vimwana, pia yale makahaba,
 jullie verorberen jonge meiden, ook de prostitués
Wanafunzi namba one, kwa utoaju wa mimba
 leerlingen jullie staan nummer een wat betreft zwangerschaps-
 onderbreking

10.

Mdawa yanayoleveya, nayo mnaendeleza,
 jullie gaan door met drugs gebruiken
Matendo ovyo mwafanya, kimasomo mwajikwaza,
 jullie vertonen slecht gedrag, jullie struikelen in jullie problemen
Mnauchezea mwanya, mimba mnazo wajara,
 je speelt met de mazen in het net, je bent zwanger
Wanafunzi namba one, kwa utoaju wa mimba
 leerlingen jullie staan nummer een wat betreft zwangerschaps-
 onderbreking

11.

Moja ninalo waomba, mlipokee kwa haki,
 ik heb terecht een verzoek aan jullie
Acheni yenu mahaba, mapenzi yasiwe keki
 hou op met prostitutie, liefde is geen cake
Hakuna mnachoshiba, ni magonjwa na dhiaki,
 laat het klaar zijn met ridicule ziekten
Wanafunzi namba one, kwa utoaju wa mimba
 leerlingen jullie staan nummer een wat betreft zwangerschaps-
 onderbreking

12.

Nimetoboa tobo, naenda zangu nyumbani,

Ik ben uitgesproken en ga naar huis

Yote nimeshachomoa, nimeweka adharani,

ik heb alle al duidelijk gezegd, ik heb gewaarschuwd

Tambia Hiyo ondoa, masomo zingatieni,

Volg de lessen die jullie gehoord hebben

Wanafunzi namba one, kwa utoaju wa mimba

Leerlingen jullie staan nummer een wat betreft zwangerschaps-
onderbreking

Shairi 5

Aids kikomo cha wazinzi ‘Aids het einde van overspelplegers’

1.

Aids mahabusi, Ugonjwa kama ajali,

Aids gearresteerde, een ziekte als een ongeluk

Unawaua waasi, wazinzi wasio jali,

doodt rebellen, overspelplegers die niet opletten

Kama wewe ni mkasi, Ukimwi wembe mkali,

Als je seks¹⁹³ hebt, is aids als een scherp mesje

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi.

Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

2.

Gonjwa lisilo na tiba, dawa kinga wa la chanjo,

de ziekte kent geen behandeling, medicijnen of een beschermend
vaccin

Ikumbukeni Bukoba, miji mingi ni magonjo,

denk aan Bukoba, veel steden zijn ziek

Vijana akina baba, walinaswa kwa muonjo

Jonge mannen, iedere man, kreeg aids

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi.

Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

3.

Aids ni adhabu, kwenye dunia ya sasa,

Aids is een straf in de huidige wereld

Umekuja kuadhibu, wale wapenda anasa

hij komt diegenen straffen die van pleziertjes houden

Hauna rika la babu, akijidai kutesa,

er blijven geen mensen meer over als hij komt martelen

¹⁹³ *mkasi* betekent in SS ‘schaar’ en in LyM ‘seks’

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi.

Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

4.

Wanaovunja amri, isemayo usizini,

Zij die de geboden overtreden waarin staat: pleeg geen overspel

Wengi wamepata shari, wamezikiwa kaburini,

Velen kregen met het kwaad te maken, ze liggen nu in graven

Tayari wanasubiri, hukumu yao motoni,

zij hoeven niet te wachten, ze zijn veroordeeld tot het vuur

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi.

Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

5.

Na, wapo wanaosema, hawaogopi ugonjwa,

En zij die zeggen niet bang te zijn voor de ziekte

Kuzini hawatatema, watachinjwa watachinjwa,

en overspel plegen, zij zullen in mootjes gehakt worden, gesneden, gesneden

Hao watu ni vilema, kiakiri wamepunjwa

Die mensen zijn gehandicapt, ze komen bedrogen uit

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi.

Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

6.

Ole wenu matajiri, na wakwasi wenye mali,

Och jullie rijken, en zij die vele bezittingen hebben

Mnao tamba dhahiri, bila hata kujijali,

Jullie die trots voortstappen, zonder je zorgen te maken

Mnawawanya vigori, pamoja na wanawali,

Jullie hebben onrijpe meisjes en jonge huwbare vrouwen

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi.

Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

7.

Mwawakatia vitita, vingi visivyo idadi,

Jullie veroveren ontelbaar velen

Mtoto bila kusita, kwako anabisha hodi,

het kind klopt zonder aarzelen bij je thuis aan

Gonjwa likisha mpata, kueleza hana budi,

het hoeft niet uitgelegd te worden, welke ziekte jullie oplopen

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi.

Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

8.

Mtoto ataeleza, ugonjwa kapata wapi,
 Het kind zal uitleggen hoe je de ziekte opgelopen hebt
“Boss” kanibembeleza, akanipa ngapi ngapi,
 “Meneer” heeft mij verleid, hij betaalde me heel veel
Kumbe Boss ameoza, kumsema siogopi,
 meneer nam me tot vrouw, ik schroom er niet voor dat over hem te
 zeggen

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi
 Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

9.

Gonjwa likisha kushika, matokeo utaona,
 Als je de ziekte hebt opgelopen, kun je de resultaten zien
Kuharisha kutapika, na vidonda kutoona,
 diarree, overgeven, en wonden die niet genezen
Homa hazitakatika, na mwisho kukondeana,
 koorts die niet weggaat, en uiteindelijk afvallen

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi
 Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

10.

E nenda hospital, watu walivyo nyauka,
 Ga naar het ziekenhuis, mensen zijn er uitgedroogd
Miili yao kwa kweli, imekwisha kongoroka,
 hun lichaam, werkelijk waar, is helemaal op
Wengine hawana hali, vitandani wanabweka,
 weer anderen hebben geen conditie, ze liggen in bed

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi
 Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

11.

Acheni yenu masafa, msiende ovyo ovyo,
 hou op met jullie gedrag, gedraag je niet risicovol
Umalaya siyo sifa, mimi nawaasa hivyo
 prostitutie is niets prijzenswaardigs, ik adviseer jullie dit
Kama unataka kufa, jifanye wewe Cossovo,
 als je dood wilt gaan, gedraag je rampzalig¹⁹⁴

Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi
 Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

12.

Tama hapa kituoni, shairi nafupishia,
 ik beëindig deze voorlichting, het gedicht kort ik in

¹⁹⁴ Cossovo (LyM) verwijst naar de Kosovo oorlog 1996-1999.

Wa juu mngoje chini, wa zama walitwambie
 iedereen heeft het voortdurend gezegd
Hili ni jambo yakini, hata tukilipimia
 een ding is zeker, zelfs als je je laat testen
Aids mahabusi ni kikomo cha wazinzi
 Aids, gearresteerde, is het einde van overspelplegers

Appendix 5 Ngonjera

Ik vat in vertaling ieder vers in een zin samen en daarna vat ik het hele toneelstuk samen, waar B ‘burgers’ zijn en V ‘voorlichters’

Ngonjera 1 Saa Nane

1. *Saa nane mkutano, wananchi eleweni,*
 B: kondigt bijeenkomst aan.
Mwembeni makutano, kwa pamoja mfikeni,
Wageni wa mkutano, wanatoka taifani,
Mahudhurio ni muhimu, usifika jela atoe (gelach)
2. *Muda utakapofika, wageni tuwapokeeni,*
 B: vraagt aandachtig te luisteren
Utulivu twautaka, usalama nayo amani,
Vifijo vikisikika, ni mapokezi kwa wageni,
Wageni na ndio hao, tayari wamewasiri.
3. *Muda bila kupoteza, utambulisho natuweni, (mwenyeji)*
 V: stellen zich voor
Kushoto ni mama Roza, kulia ndiye Amani,
Wa tatu ndiye Muhoza, anatoka taifani,
Karibu wageni wetu, mwongee na wananchi.
4. *Wageni samahani, nasi tujitambulisheni, (mpinzani)*
 B: stellen zich voor
Tex namba wani, wa pili ndiye Fauni,
Mwingine ndiye Tauni, na mimi ndiye Amuduni,
Nafasi nawadihieni, utambulisho nimemaliza.
5. *Ndugu zangu sikieni, habari njema pokeeni, (mgeni no 1)*
 V: hiv-virus is dodelijk
Dunia i taabani, wananchi eleweni,
Atakae pona nani, swali nawaulizeni,
Vijidudu vya HIV, hakika vitatimaliza.
6. *HIV vinatisha, ni vema mkaelewa, (mgeni no 2)*
 V: onveilige seks leidt tot dood
Maisha vinakatisha, wauni wanauwawa,

- Mapenzi mkidumisha, kaburini mtafukiwa,
Vijidudu hivyo hatari, ukigusa utanata.*
7. *Vijidudu hiviyo hatari, wananchi epukeni, (mgeni no 3)*
V:virus is dodelijk
*Heri ufe kwa kisukari, ndugu watakutamani,
Ni bora uwe baini, ngono bila utani,
Ukitaka ubaki ufito, fanya ngono nzembe uone*
 8. *Inzi kufa kwenye kidonda, hakika siyo haramu, (mpinzani 2)*
B:iedereen gaat dood
*Virusi vikutuponda, hatuwezi kulaumu,
Utavuna ulichopanda, hilo wewe ufahamu,
Kumbukeni klia mtu, kubarikiwa kifo chake.*
 9. *Ni wengi wametambua na leo hatuwaoni, (mgeni 1)*
V:virus is dodelijk
*Walifanya mahaba, dunia kuipondeni,
Virusi vilipowakala, wali kandamizwa kaburini,
Raha itapogeuka, na nyinyi mtaomba sala.*
 10. *Tex nasimama, kauli kuitoweni, (mpinzani 3)*
B: liefde is van alle tijden
*Hakuna cha lelemama, dunia twaipondeni,
Fauni wangu daima, napitia ubavuni,
Hata wale wa zamani, walikuwa mtu na wake*
 11. *Hata iwe kwa mtutu, kamwe hatutateleza, (mpinzani 4)*
B:ieder gaat dood
*Ni shuguli na mtu, ubaya kuendeleza,
Asikie kila mtu, wanakijiwe twaeleza
Mbona yesu alikufa, sembuse mimi na wewe?*
 12. *Mpende na msipende, Juliana anatisha, (mgeni 2)*
V: aids is dodelijk
*Mapenzi siyo makande. Mseme mtayashiba,
Hata wale wamekonda, si mchezo wanakwisha
Epukeni usherati, gonjwa hili ni balaa.*
 13. *Yote mnayoyanena, hayafai hata kidogo, (mpinzani 1)*
B: we geloven geen woord
*Washori ni danadana, kwa mapenzi tu vigogo,
Na fedha tutazichana, mademu tunao usongo?
Hatuna kazi mbadala, acheni dogo watuuwe*
 14. *Ngono mnazoeneza, ipo siku mtajuta (mgeni 3)*
V: vermijd overspel
Na dogo mnaotukuza, kamwe hamtawapata

- Mitaani watawabeza, gonjwa likishawakita,
Epukeni usherati, msije mkwuwa nao.*
15. *Kamwe haturudi nyuma, ni mbele tutanasonga, (mpinzani 2)*
B: prima om heldhaftig te sterven
*Wenye kuona na kusema, hao watajigonga,
Dogo na akina mama, hapa watjipanga,
Bora ufe kishujaa, uzitimize amuni? Of ahadi*
16. *Mapenzi ni kama pipi, hilo twafahamisha, (mpinzani 3)*
B: Liefde is snoep, vriendin troost
*Na kukonda kama pipi, siyo jambo la kutisha,
Fauni wangu fupi, ni tulizo la maisha,
Au vipi mtu wangu, wasemayo ni Ulawiti*
17. *Mauti yakiwafikia, jeuri utawaisheni, (mgeni 1)*
V: toegeven aan begeerte leidt tot dood
*Mfupa mtabakia, inchi kumi kiunoni,
Dunia mtaichukia, sijui mtalaumu nani,
Tamaa ongeza ulafi, jibu lake ni mauti.*
18. *Ugonjwa hilu ni tata, ni vema mkiepuka, (mgeni 2)*
V: vermijd deze rampzalige ziekte
*Hakika ukikupata, jihesabu umeondoka,
Mwilini ukijikita, utabaki kudhoofika,
Juliana mwisho wa yote, kwa kutibua namba one.*
19. *Ni gonjwa la kawaida, sisi shida hatuoni (mpinzani 4)*
B: aan deze ziekte is niets bijzonders
*Roho haziwezi kudunda, gonjwa mkilitamkeni,
Tex ni langu tunda, ametulia rohoni,
Dunia hii ni watu, na watu ndio sisi*
20. *Hatuchoki kuwambia, enyi wetu waungwana, (mgeni 3)*
V: ziekte richt ten gronde
*Mapenzi mkikalia, virusi vitawabana,
Mwilini vikitulia, polepole vijatafuna,
Asiye sikia la Mkuu, huvunjika guu lake.*
21. *Wadogo zangu nyanyuka, baba dada pia mama (mpinzani 1)*
B: erkent gelijk voorlichters
*Janga hili kuepuka, ni jambo la heshima,
Msije mkapofika, mautini mkazama,
Hakika mkita pema, pabaya panamuita.*
22. *Tunarudi siyo utani, tusije tukaangamia, (wapinzani wote)*
Alle burgers: ze hebben gelijk
*Ukweli tumbaini, msemayo ni usia,
Virusi viko mbioni, vinapiga makasia*

*Tunaomba tushikamane, janga tulitokomeze
 (watapiga makofi kuashiria mapokezi) wote
 Ni kilele tumefika, nyote mmesikia,
 Burgers en voorlichters: verander gedrag
 Mengi tuliyotamka, muhimu kuzingatia,
 Mapenzi yakifanyika, gonjwa litatokomea,
 Gonjwa hili kinga yake, ni wewe kubadili tabia*

Samenvatting: Een vertegenwoordiger van de burgers roept burgers op om naar de bijeenkomst te komen waarin gasten (voorlichters) info over aids komen geven. In dit toneelstuk komen beurtelings beide partijen aan het woord, waarbij de voorlichters telkens weer aankondigen dat ‘casual’ seks tot de dood leidt en de burgers benadrukken dat ze er niets van geloven, dat seks van alle tijde is, en dat de geliefde rust geeft. Op het einde erkent een burger dat de voorlichters gelijk hebben en maant zijn vrienden de boodschap aan te nemen. Dit doen ze en allen zeggen dat ze de boodschap geloven. Het toneelstuk eindigt met de oproep – door ‘voorlichters en burgers’ uitgesproken- om de ziekte te vermijden en gedrag te veranderen.

Ngonjera 2 Mama na Familia

1. *Mkutano, mkutano, wajumbe msichelewe,*
 Burger roept jongeren op voor bijeenkomst
*Saa ndizo hizi, vijana, watoto jamaa,
 Huu ndio wakati wa kujikangonja*
2. *Ninasikia makelele, na mambo yasomaana,*
 Burger kondigt aan dat daar te leren valt
*Si hapa wala kule, watu wasemezane,
 Wacha chake kieleele?, la sivyo tutakosana,
 Mikutano ya klia siku, maana yake ni nini?*
3. *Wewe kaka yangu Toma, naomba uache matusi*
 Burger herhaalt oproep
*Anayeturla ni mama, ataka kuongea nasi,
 Na mimi amenituma, anaoujumbe makususi,
 Twende katika baraza, tukae na tubasizi,*
4. *Wana chukueni viti, mbarizi kukalia,*
 Burger kondigt aan dat het over aids gaat
*Yametufika mauti, kaeni niwape wosia,
 Kuna gonjwa la utiti, la ukimwi mwaambia,
 Wanangu mnisikilize, mjitunze mtaishi*
5. *Ujana ni Moshi vile, na katu hautarudi,*
 Burger vraagt aandacht

- Nyanya alikuwa kule, na yu wapi hajarudi*
Wana ondokeni kule, kwenye raha na ufigadi,
Dunia Tambua? bovu, wanangu muwe makini
6. *Wewe yako yamepita, tuache wakati wetu,*
 Oproep te luisteren om geen aids te krijgen
Ukimwi si utapita, kama mengine mametu,
Wakati umepita, huu sasa ndiyo wetu,
*Mla ni mla leo, mla jana kala nini.*¹⁹⁵
 7. *Ni wengi walisema hivyo, ujana ukiwasukuma,*
 Bij onveilige seks is virus dodelijk
Mapenzi wakifanya ovyo, tamaa nyuma,
Walifanya watakavyo, virusi vikawauma,
Majuto yakaja nyuma, baada ya kuharisha
 8. *(mama) Doli komu ni mimi, maisha raha na huni?*
 Vrouw: ik zie geen mooie dingen
Wataka nambia mimi, niache kuona nini?
Sema wengine si mimi, mimi sioni uzuri,
Mla ni mla leo, mla jana kala nini?
 9. *Nawanangu mapinduzi, dunia sasa i taabani,*
 Vrouw: de wereld heeft een ernstig probleem
Maisha ya siku hizi, si kama ya zamani,
Inabidi ukaye uzi, akiliziwe masomoni,
Vinginevyo mwanangu, nazi haishindani na jiwe
 10. *(mama) Maisha ya siku hizi, ni ya raha na unono*
 We hebben tegenwoordig een goed leven
Tungi kwangu ndiyo kazi, na wangu muitakano?
Sisi hatuvaa ngozi, mama wacha maneno,
Mla ni mla leo, mla jana kala nini?
 11. *Enyi watoto wa kakangu?, msiwe kama wenda wazimu*
 Aids is vergif
Dunia sasa ni chungu, Ukimwi sasa ni sumu,
Mkifunikwa ukungu, mtabaki kujikumu,
Heri nusu ya shari, kuliko shari kamili
 12. *Ushauri sasa ni bure, gharama ni matibabu,*
 Gedraag jullie netjes
Enendeni makelele, mkasomee matibu,
Heshima wekeni mbele, mjifunze kwa adabu,
Mnenayo yamepita, leo mbwembwe za nini?

¹⁹⁵ Het spreekwoord *Mla ni mla leo, mla jana kala nini?* Vertaling: hij die vandaag eet, eet vandaag, hij die gisteren at wat betekent dat? Betekenis: hij die vandaag iets bezit wordt gerespecteerd, niet degene die gisteren iets bezat (Wamitila, 2001).

13. *Shangazi watuambia nini, eti tuenzi ya mababu,*
 Jongere: moeten we ons als onze voorouders gedragen?
Tutapaje wana ndani, tukiwa kama mabubu,
Tuacheni tufue fani, tuutimize wajibu,
Maji ni mla leo, mla jana kala nini?
14. *Zama zile za kale, tulikuwa tukione,*
 Vrouw: jeugd kent geen respect meer
Watoto heshima tele, nyumbani kuelewana,
Leo hii kiburi mbele, watoto heshima hawana,
Mkiiga munya kwa tembo, mtapasuka msamba
15. *Sikilizeni watoto, akili ziwe timamu,*
 Vrouw: vermijd drugs en overspel
Epukeni misokoto ya bangi kwenu simu,
Bora mponde kokoto, maisha yawe matamu,
Uasherati na Ukimwi, ni mbaya ilyokaangwa
16. *Epukeni vishawishi, vya marafiki wabaya*
 Vrouw: vermijd slechte vrienden en verleiding
Kuweni na utashi, wa kuvunja ukimya,
Uacheni ubishi, mkasome kama kapyu,
Msiposikia la mkuu, mtavunjika guu
17. *Hakika si uzandiki, hayo mliyoyesema,*
 Jongere; ik ben het met mevrouw eens
Nimeacha unafiki, na ukweli unauma,
Na yule asiyesadiki, aendeleze tuhuma,
Binafsi nimekubali, sijui vipi wenzangu
18. *Hakika mkita pema, pabaya panamuita,*
 Jongere: ik stap uit problemen en laat me onderwijzen
Hata mimi nimepima, nikaondoa utata,
Aliyoyasema mama, akilini yamekita,
Asiyefunzwa na mama, hufunzwa na ulimwengu
19. *Hata mimi siko mbali, nimejifunza kitu,*
 Andere jongere: ik ben het er ook mee eens
Ushauri nimekubali, nimeacha utukutu,
Nitaanza na kusali, mapenzi sitathubutu,
Ukimwi sasa ni basi, sibipu wala sipigi
20. *Ukimwi kweli ni janga, hata mimi nimeamini,*
 allen: aids is een ramp, we hebben religie nodig
Linaua hata wajinga, waasi na waumini,
Nimeamua kujiunga na wenzangu kanisani,
Bila msingi wa dini, Ukimwi utatimalize

Samenvatting: een vrouw spreekt jongeren toe. Ze maant hen zich beter te gedragen: geen drugs gebruiken, slechte vrienden te vermijden. Na aanvankelijke bezwaren van de jongeren, geven allen toe dat de vrouw gelijk heeft.

Ngonjera 3 Janga hili la Ukimwi De ramp die aids is

Janga hili la Ukimwi watu tujihadhari

In dit vers discussiëren een aantal mannen of aids echt wel een ramp is. Uiteindelijk gaat men akkoord naar de vergadering te komen

1.

Umaskini jamani, ni kitu kibaya sana, (Majuto)

Kitu hiki umaskini, mfano wake hakina,

Na tena umaskini, katu heshima hauna,

Ni wapi tutakapokwenda, ni wapi tukimbile?

Mie mwana wa tikiti, niendepi nifarijike? (Majuto)

Nitasagika tikiti akile ziparangane

Mzee mwenzangu vipi, waenda wajisemea, (Bwana Kiboya)

Nambie tusaidiane, leo kwako kesho kwangu

Ndugu, shida taab na balaa zanitia kero kubwa (Majuto)

Umaskini mwanzangu ni taabu yaniumbua

Sikiza nikwambie, utulie kwa makini, (Bwana Kiboya)

Ukweli ungundue, uyaingize moyoni,

Ndipo nawe utambue, mpate aheni,

Umaskini si tatizo, tatizo ni hili gonjwa

Ukimwi bwana Majuto, ni janga lijadiriwe (Bwana Kiboya)

Vijana wetu wa sasa, muhimu wasaidiwe,

Wazazi inatupasa, wiziwazi waambiewe,

Tukisha kufanya hili, vijana tutawaponya

Tusiandikie mate, na wakati kuna wino, (Bwana Kiboya)

Nakuomba usisite, usiji kosa unono,

Na pale kwa ndugu Makote, kipo kikaa saa tano,

Cha husu gonjwa hatari, mbinu gani zitumike

Ahsante bwana Kiboya, Ahsante ndugu Udumu, (Majuto)

Macho umenifumbua, kuniambia ya muhimu,

Leo sasa nimejua, tatizo kubwa muhimu,

Tuwahi mkutanoni, janga hili liamba

2.

Voorzitter roept oude en jong, alle mensen op vergadering bij te wonen

Jamani ndugu zangu, wazee wenzangu, (M/kiti)

Wazazi wenzangu, watanzania wenzangu,
 Napenda niwaweke sawa, ili twende sote sawia, (M/Kiti)
 Ndiyo-taarifa mliyopewa, wito mkaitikia
 Lakini-akili jama ni nywele, kila mtu ana zake
 Enyi wazee wenzangu, naomba tusikilizane, (M/Kiti)
 Kwa kawaida wenzangu, wazee, ndio wenye nchi,
 Bila waze nchini, nchi itayumba sana,
 Lengo la hiki kikao, twataka tujadiliane
 Tujadiliane hasa, kuhusu gonjwa Ukimwi, (M/Kiti)
 Oneni vijana sasa, maisha wapukutika,
 Jukumu letu kwa sasa, ni dawa kuitafuta,
 La sivyo ndugu zangu, nchi itabakia wazee
 Mie naketi kitini, nizekaribishe hoja, (M/Kiti)

Voorzitter roept om meningen te uiten
 Toeni yenu maoni, fursa kila mmoja
 Tena tuvumilianewala pasipo ghadhabu,
 Nafasi sasa i-wzi, tuanze kuchangia.
 Mwenyekiti shukrani, kwa mwanya kunipata, (Koroso)

Koroso (toehoorder):
 Raakt de ziekte alleen jongeren?
 Mie ninayo maoni, naomba kusaidia
 Swala la huu ugonjwa umma kusaidia
 Hivi ni kwa vijana tu, au na hata wazee?
 Kwa utazamo upana, wazee nao hawalali, (Koroso)
 Fumbo fumbia mjinga, mwerevu huling'amua,
 Wakeni mambo bayana, hatuitaki mizungu,
 Miye mwana wakopoka, tusitake kufumbafumba.
 Koroso wa kupoka, sikiliza nikweleze, (Katibu)

Secretaris:

Ziekte raakt ook ouderen, maar jongeren zijn steunpilaar van de
 maatschappij en ze hebben nog vele jaren voor zich
 Mwenyekiti kutamka, vijana wasaidiwe
 Siyo kwa maana kwamba, hawahusiki wazee,
 Ila vijana nguzo ya nchi, nchini wategemewa.
 (Isitoshe), Vijana ni rasilmali, ya hili letu taifa, (Katibu)
 Na tena vijana bado wangali, na miaka mingi mbele,
 Wana visawishi vingi, wepesi wa kudanganyika,
 Twaomba tuendelee, kutafuta ufumbuzi

Wazee tukumbuke, Ukimwi si lelemama, (Karani)

Klerk:

Aids is geen spel laten we luisteren

Chonde Chonde twamke, tusijitwishe lahama,

Tumekuwa na makeke, ya nyuma tumeyahama,

maendeleo haya yanatumiza vichwa

Zama zile za kule, tulikuwa tukiona, (Karani)

Mwane na mzazi wake, wakikaa kukomeni,

Walipewa maadili, kwa vitendo na mifano,

Leo eti maadili, wayapata kwa vuninga

(Jamani) tuchekeche kwa undani, kisha dawa tuitoe, (mama Sara)

Voorlichter:

Voorlichters benadrukken dat meisjes te veel vrijheid hebben om

lang op straat te flaneren

Aliyoyasema kalani, ni ukweli tugundue,

Wazazi hatuna muda, wa kukaa na wanaliletu (?)

Ushauri hatuwapi, tumeiachia dunia

Jingine baya zaidi, ni hili lisikieni,

Mabinti zetu wa kike, wana uhuru mkubwa,

Kutwa kucha mitaani, wafanyachio ukioni,

Mchana hadi jioni, hivi hupika saa ngapi

Mambi haya ni mazito, jama tuyape uzito, (Mzee wa Busara)

Toehoorder

Vraagt uitleg over ziekte en benadrukt belang van godsdienst

Yatatujia majuto, tubakie kama fito,

Tusiya fanye kwa mkato, tushindwe kuvuka mto

Imefikia wakati, dini tuiangalie

Watoto watizameni, kwa jinsi wanavyovaa, (mzee wa Busara)

Mimi niwaulizeni, ni wapi kule wakaa?

Mipasuo matakoni, eti hii ni Tanzania,

Tuachie wayiroa wakatulelee wana

Kwa zinaa kushamini, kuna vishawishi vyake (Mzee Busara)

Uhuru umekithiri, serikali istuke,

Picha zaleta dosari, serikali izimlike,

Janga hili la Ukimwi, watu tujihadharini

Tangu mwanzo mmenene, kuhusu vijana wetu, (Mzee Haruni)

Toehoorder

Als man en vrouw niet samen zouden slapen dan zou alles voor niets

zijn

Mawazo mloyanena, yote jama madhubuti,

Lakini nami ninayo, nadhari yatatujenga,

Jukumu hili ni kubwa, mpaka tufunge kibwebwe
 Mmeeleza chanzo, cha tatizo la Ukimwi, (Mzee Haruni)
 Ila ufumbuzi wake, hakuna aliyeutoa,
 Hivyo miye ninasema, tuwajengeni vijana,
 Tuwape mwanga wa dini, wawe na Mungu moyoni,
 Bila msingi wa dini, twatwanga maji kinuni, (Mzee Haruni)
 Dini ndiyo yetu kinga, ikianzia shuleni,
 Mungu tumtafuteni, hili tuzingatieni,
 Hakuna kinga nyingine, Mungu kinga peke yake
 Wanetu tuwa ketishe, tuwaelezeeni bayana, (Mzee Haruni)
 Mbinu zote tufundishe, wazi bila kufichana,
 Zaidi tuhakikishe, baba mama kuungana
 Tusipokuwa wamoja, itakuwa kazi bure
 Acheni mie ninene, niondoe dukuduku, (Mawazo)
 We sterven door een ramp
 Inasononesha sana, inasikitisha sana,
 Ni nini hasa maana, nchi kuwa konakona?
 Hivi watanzania ni wapi tunakokwenda?
 Zinaa nyakati hizi, kweli ina mwanya kweli,
 Chekecha utafakari, kama unazo akili,
 Ni nani hufurahia, anapobugia sumu?
 Anyeshe mkono wake ikibidi apongezwe
 Nataka kusema kitu, imefika mahali, watu tukaelimika, (Mawazo)
 Imefika mahali, kuzingatia kanuni,
 Imefika mahali, kujali maelekezo
 Kama jama hivi ndivyo tutakufa kipumbavu.
 Tabia za kizamani, mbali tuzifutilie (Mawazo)
 Voorlichter
 Injectienaalden, delen van borden en ontrouw zijn gevaarlijk;
 Sindano za mitaani, ni hatari tusikie,
 Vyombo vya kutahiria, daima tusichangie,
 Na kisha katika ndoa, tuweni waaminifu
 Epuka kulandalanda, penye sehemu hatari, (Mawazo)
 Vermijd gevaarlijke, verleidelijke plaatsen
 Mitaani vitabuni, ni maeneo hatari,
 Penyemiziki dansini, ni vishawishi hatari,
 Ndiyo yangu mwenyekiti, yapeni kipaumbele
 Kwa vijana tumenena, kinga yake tumepata, (Baruti)
 Voorlichter
 Man en vrouw leven er op los. Dit is een groot gevaar
 Mawazo tumeungana, tukaujua utata,

*Lakini ninaungana, na wzo lake mawazo,
 Shilingi tuigeuze na kwa upande wa pili.
 Wana ndoa sikilizeni, msizibe masikio, (Baruti)
 Twaishi kama wahun, hatuna mwelekeo,
 Mume na mke ndani, hatuishi kwa upendo,
 Sasa kama hivi ndivyo twaitafuta balaa
 Kasoro ndani ya nyumba, hatari yake ni kubwa, (Baruti)
 Tutaruhusu kuyumba, shetani kucheza kubwa,
 Wana ndoa mkiyumba, na watoto watakumbwa,
 Hali ikishamiri, umeruhusu Ukimwi
 Wenzangu mmepapasa, tatizo kuligundua, (Kitimoto)*
 Toehoorder
 Ik ben geraakt door jullie woorden
 Chanzo cha yote hasa, mimi nitawaambia,
 Hakika litawagusa, moyoni litawaingia,
 Kuranda bila ya kazi kwa sababisha balaa
 (Kwa mfano)
 Kimwana huyo anapita, kijiweni mmekaa, (kitimoto)
 Mbwata mbwata mbwata mbwata, nyote jicho mwatupia,
 Ni nini kitakachofuata, kama si kuzengea?
 Ungelikuwa kazini haya yangelitoka wapi?
 Janga hili niwambie, lataka tuzingatie,
 Wazazi wafikirie, na umma ufikirie,
 Kila mbinu tutmie, mgonjwa dawa ainywe,
 Marufuku itangazwe, vijana wasizagae
 (Mwisho ni hivi)
 Serikali twaiomba, iimarishe vikundi, (Kitimoto)
 We vragen de overheid hulp
 Mara hadi kule pemba, vikaene vikundi,
 Vilime nyanya na pamba, kwa kilimo cha kifundi,
 Hili likishamiri, utapungua Ukimwi.
 Wajumbe ninawashukuru, swala kulifanikisha, (M/kiti)
 Voorzitter bedankt
 Bila kufanya kukuru, jambo tumekamilisha,
 Sasa tubakie huru, wanai kuwafundisha,
 Ahsanteni waungwana, heri ninawatakia.

Samenvatting: De voorlichters benadrukken het gevaar van aids niet alleen voor jonge mensen. Ze richten zich tot hen omdat ze de steunpilaren van de maatschappij zijn. Jonge meiden zouden te veel vrijheid krijgen en man en

vrouw gaan vreemd. Publiek is van mening dat het normaal is dat man en vrouw samen leven. Uiteindelijk erkennen ze gevaar van aids.

Ngonjera 4 Kwa Heshima

1. *Kwa heshima taadhima, twaja kwenu walimwengu (ushauri)*
 Voorlichters: We komen jullie advies geven over het grote verdriet 'aids'
Ushauri twawatetea, msije kuwa wachungu
Tumevamiwa jambazi amejawa na machungu
Jambazi huyu Ukimwi tishio ulimwengu
2. *Pande zote za dunia amesha kita mizizi (ushauri)*
 Aids gaat verwoestend te werk
Saini ameitia, Gaidi huyu nyambizi,
Huyu hana lelemama kila siku kwake kazi
Jamani tujiadhari Ukimwi utamaliza
3. *Ukimwi mnasema hivi chanzo chake nini, (upinzani)*
 Publiek: Aids wordt veroorzaakt door hekserij. Ik geloof het verhaal over aids niet
Tena umetoka wapi tafadhali nielezeni,
Hayo ni mawazo potofu mnayotwambieni,
Ninyi wauwa? Ndio wachawi mnaotuuweni
4. *Machoyeme mekundu ushauri umewakoleeni, (upinzani)*
Mkisha tudhoofisha Ukimwi mwasingizieni
Kwangu hizo ni adithi sawa naza redioni
Hayo msemayo siyaelewi labda twanze mengine
5. Voorlichter: Aids richt ons ten gronde
Ndugu yangu kitania sikiliza (ushauri)
Maisha twayachezea ngono kwa kuendekeza.
Ukimwi twajizolea, maisha twayakatiza,
Yatupasa kutulia Ukimwi utatuma,
Tusipochukua taadhari Ukimwi utatuma.
6. Voorlichter: Ieder begrijpt dat thee zoet is; het achterwege laten is moeilijk. Aids richt ons ten gronde
Chai ilikuwa tamu, kila mtu aelewa (ushauri)
Kwa sasa imetiwa sumu, tukionja tuta uwawa
Kuacha isiwe ngumu, mauti tusije patwa,
Jamani tujiadhari Ukimwi utatuma.
7. *Mnayosema nayasikia, lakini sitowakubalia, (upinzani)*
 Publiek: Ik ben het er niet mee eens. Mooie meiden brengen mij rust. Ik laat seks niet achterwege. Er is niets leuker dan seks.
Vimwana nitavisaka, kwenye getho vitatulia

Mtoto Englishi figer? Miguu yake ya bia

Eti mwasema tuviache ng'o mimi siachi

8. *Kimwana kama huyu (upinzani)*

Kifuani akitua, joto asimilia tisini,

Denda akinipiga, na busus kulitoeni,

Kabati akinifungulia, raha nyingine sioni,

Hacha uniwe, dogo dogo siachi.

9. Voorlichter: Mannen richten jullie ten gronde

Jambo nililogundua, wanaume mnatisha (ushauri)

Matako wakitikisa, uume mwasimamisha

Msululu mtajipanga, hodi hodi mkibisha,

Kweni wenye mitazama, la sivyo mtakwisha

10. Voorlichter: Jullie oude mannen: droom slechts

Nanyi wazee msije moto, wenye busara kuweni, (ushauri)

Mtakuja chomwa moto, vibinti mkivipendeni,

Mwasema eti vinajoto, tena eti viko makini,

Kama mnapenda joto, kwa nini msiote moto

11. Publiek: Meiden zijn vruchten waar we van willen genieten

Neno ninalowambieni, kila nafasi itaonja mauti (upinzani)

Tie usitie kaburi utaketi

Hebu niambieni wapi tuwapeleke mabinti

Hapa ni matunda yetu lazima tuyafaidi.

12. Voorlichter: aids is dodelijk

Ukimwi mnaousema ni ugonjwa sawa na homa (upinzani)

Hata usipokufa kwa ukimwi, hakika utakufa kwa homa

Mseme msiseme, vimwana vitanikoma

13. Publiek: God heeft gezegd: vermenigvuldig u

Neno ninalofahamu ni hili (upinzani),

Mungu alisema zaeni mwongezeke,

Tena ndio kisa kaumba mme na mke,

Leo mnasema mtutenge wanawake

Je, tutaongezekaje bila--- (onyesha katia)

14. Voorlichter: God heeft gezegd trouw te zijn

Ni sawa lakini---sikiliza basi (ushauri)

Mungu alisema mke na mme wawe waaminifu

Tena hakuumba mme na mke kwa uzinifu

Hoja mnayoitelea hakika ni mufu

Tafadhari naomba tuungane ili tumshinde nyambazi

15. Voorlichter: Onveilige seks richt jullie ten gronde en niet magie

Kukulu kakala kwenye mihogo, ngono mmefanya keki (ushauri)

Chomolea vichocholoni, kwenu mukiki mikiki

*Tena mwachoma pekupeku, salama bila jalini,
Ukimwi ukiwabana, mnasingizia mmelogwa.*

16. Alle mensen uit publiek. We erkennen het gevaar van seks

Hakika tumepotea njia tumeicha (upinzani waungani)

Tutakuja kujitia ushauri tukiacha

Tuungane pamoja ngono nzembe kuziacha

Waungwana tupokeeni, tulikuwa tumepotea

17. Allen: Als we niet voorzichtig zijn richt aids ons ten gronde

Hapa mwisho tumefika, ushauri tumewapeni, (mwisho)

Watakaodharau ushauri, ukimwi utawabaneni

Na watakaojifanya ng'angali, nyambizi atuwaweni,

Tusipojiadhari Ukimwi utamaliza.

Samenvatting: De voorlichter blijft het risico van onveilige seks en aids benadrukken. Het publiek-jonge mensen- geven aan dat magie de oorzaak van de ziekte is en niet seks. Seks en jonge meiden zijn om van te genieten en dit is van oudsher zo, benadrukken de jongeren. Uiteindelijk gaan de jongeren akkoord met het standpunt van de voorlichters dat onveilige seks gevaarlijk is

Appendix 6 Rapu, Rap-liederen

De dikgedrukte woorden in de teksten zijn straattaalwoorden.

Rap 1.

Kinga 'Protect'

Chorus:

1. *Ahaa. Wazee wa 18 washa moto*

Ahaa. Elder men of 18 light a fire

2. *Ahaa. Wazee wa 18 Piga **ngetwa** 2 x ahaa*

Ahaa. Elder men of 18 local medicines x2 ahaa.

3. *Sijui alikotoka huyu **DEMU***

I do not know where this female lover comes from,

4. *Sijui alikotoka **MENI**, mara ya kwanza kinga¹⁹⁶*

I do not know where these men come from, the first time I used protection,

5. *Mara ya pili kinga, mara ya tatu haa, ninamwamini*

The second time I used protection, the third time haa, I trusted her,

¹⁹⁶ The rappers show a condom.

6. *Huo ni ujinga kuendekeza mapenzi ya kishenzi*¹⁹⁷, *kishenzi*
It is ignorance to give in to idle sex.

Verse 1.

7. *Vijana wakimwona DEMU yuko kwa furani*,
Young men, if you see a certain female,
8. *Watazembwera zembwera utafikiri mbwa mwitu*
You follow her, like a wild dog,
9. *Au mithiri ya fisi waliojaa mstuni, utawaulumia*¹⁹⁸,
Or like hyenas who fill the forests, you can have mercy on them,
10. *Jinsi wanavyozunguka, "hawajui waufata aliye athirika"*
As they move around they do not know that the person that they
follow is infected x2
11. *Ebu cheki cheki x2. Je wajua ni mzima-zima*,
hey look, look" x2. How do you know she is healthy healthy,
12. *Je wajua amepima-pima x2 chorus*
How do you know she has been examined-examined

Verse 2.

13. *Ukimwi watumaliza jamani tujiadhari*.
AIDS will destroy us hey you people be cautious,
14. *Mzunguko wa Ukimwi tazama umekithiri*,
Spread of AIDS, look out, AIDS increases,
15. *Tutunze ndoa zetu, tuache ngono nzembe*,
Let us take care of our marriage, stop idle sex,
16. *Tutunze familia zetu tuzipe maadili mema*.
Let us take care of our family, let us behave according to good
morals
17. *Kila ninapolala mchizi naweweseka*,
Every time I sleep with a lover, I worry,
18. *Nikimwona bibi anavyo suka mkeka*,
If I see grandmother weaving a mat,
19. *Hari siyo shwari Ukimwi watumaliza x2*,
The situation is not calm, AIDS will kill you x2.
20. *Kati ya wathirika wewe unahesabika*,
You can count yourself among the infected persons.

¹⁹⁷ De schrijver M.G. Vassanji beschrijft in zijn boek 'The Gunny Sack' de herkomst van het woord 'mshenzi'. 'Even now a 'mshenzi' is a barbarian. In those days, when the coastal folk regarded themselves as the epitome of civilisation and urbanity, a Mshenzi was anyone who was not from within walking distance of the coast' (1989:14).

¹⁹⁸ *Ulumia* is here *hurumia*.

21. *Kula vizuri, fanya mazoezi, utaishi kwa matumaini x2.*
Eat good food, do your exercises, you will live with hope x2.

Verse 3.

22. *Mpenzi nakupenda, naogopa hujapima*
My dear, I love you, I am afraid that you didn't take a test
23. *Wazee wa 18 wanakupa ushauri*
The elder men of 18 give you advice
24. *KIUKAKI¹⁹⁹ inakupa ushauri x2*
KIUKAKI gives you advice x2
25. *Raba²⁰⁰ atafanya nini sasaaaa.*
Raba what will he do now
26. *Kunguru atafanya nini sasa.*
Kunguru what will he do now
27. *Roga atafanya nini sasaa....*
Roga what will he do now
28. *Kama kuelimisha wamesha elimisha x2,*
to educate, you have already been educated
29. *"Twende tukapime tujue afya zetu" x2 chorus*
Let us go for a test, so that we know our health condition x2

Verse 4.

30. *Nanyi wazee wetu ebu acheni upuuzi,*
And you elderly, hey, stop that nonsense,
31. *Mkiviona vimwana vyapita mwashusha pumzi,*
If you see pretty young girls passing, you hold your breath,
32. *Hamjui ni watoto wenu mlio wazaa,*
You do not realize that they are your children, your procreation,
33. *Mwawataka mapenzi hamjui ni ushenzi,*
You want them as lovers, you do not realize that it is barbarity
34. *Majuzi nimeenda pwani kwa mzee Machunde*
Recently, I went to the beach to see Mister Machunde,
35. *Nikamkuta huko **chemba** anakuna makende,*
I meet him, segregated, he scratches his testicles,
36. *Nikauriza wafanya nini mzee Machunde,*
I ask him what are you doing Mister Machunde,
37. *Hakunijibu, Aona aibu x2*
"He does not answer me, he feels ashamed

¹⁹⁹ Name of the performance group.

²⁰⁰ Raba, Kunguru, Roga are the rappers's names.

38. *Kumbe ameathirikaaa... Mzee na kipara chake* x2
 “Hoh he has been infected, Mister with his baldness”
39. *Kula vizuri, fanya mazoezi, utaishi kwa matumaini* x2
 Eat good food, do your exercises, you will live with hope
40. *Si ulitaka chai chai iweje lalamika unaanguaa*
 If you like tea tea, how can it be that you complain that you will be burnt
41. *Kuwa mwangalifu msikivu, mwelevu Ukipenda sana ngono*
 Be careful, attentive, intelligent, if you like sex very much
42. *Itakuwaa si ulitaka chiii iii, iweje*
 let it be, if you like tea,
43. *lalamika unaanguaa- kuwa mwangalifu msikivu mwelevu*
 How can it be that you complain that you will be burnt — be careful, attentive, intelligent
44. *Ukipenda sana ngono itakuwaa* x2 “*Itakuwaa*” x3
 If you like sex very much, let it be

Rap 2.

Ukimwi unatisha ‘AIDS frightens’

Verse 1.

1. *Jescka nilikupendaa sina shaka ila wewe waelewa-lewa*²⁰¹
 Jescka I loved you without doubt no one except you understands this
2. *Kwa penzi nilikuenzi moyo wangu ulikuwa umelewa-lewa*
 I honoured you with love my heart was drunk-drunk
3. *Hospital tulienda kwa taadhima UKIMWI tukapima-pima*
 We went to hospital with dignity to test on AIDS-
4. *Majibu yakatokea wakakuta sisi sote ni wazima-zima*
 The results were that we both were healthy

Verse 2.

5. *Yote tuliyo ongeaa; Jescka uliyaona ni ushenzi-shenzi*
 All the things we talked about; Jescka you realized that it was barbarity
6. *Kuhusu kufunga ndoa; hayo yote uliona upuuzi-uzi*
 To get married; all these things you saw them as nonsense
7. *Ulizama Kisiwani; Ukaenda kuwa pikia wavuvi-vuvi*
 You submerged on an island, you went there to prepare food for fishermen

²⁰¹ De derde persoon meervoud wordt vaak gebruikt als de neutrale derde persoon ‘men’.

8. *Leo watoa machozi- wataka mimi nije rudia nawe nawe*

Today you are crying- you want me to come back to you

Chorus

9. *Iweje leo waja kwangu mimi turudiane*

How can it be, you came to me, to ask me to start our relationship again

10. *Iweje leo waja kwangu mimi*

How can it be today you came to me

11. *Gonjwa hili jama latishaa, pande zote limeshafikaa,*

This disease, friends, destroys us, it has arrived from everywhere,

12. *Jamani tujiadhari, ama sivyo sote litatimaliza x2*

Friends let us be cautious, or the disease will finish us all x2

Verse 3.

13. *Leo hii niko **fit**-ile fit kwa mistari niko fit-fit*

Today I am fit- I am fit to give advice, I am fit

14. *Maisha sasa ni **yes mademu** wote sasa **nimewashit**-shit*

Life is now: yes, I have left all lovers now

15. *Kwangu hakuna nafasi labda ukajalibu kwa Hamis-mis Hamis-mis*

I have no place for you, perhaps you try at Hamis-mis Hamis-mis

16. *Wangu ameshatuliza²⁰² ndani wala yeye kwangu hana wasiwasi*

I am calm inside, and I have no problem at home

Chorus.

Verse 4.

17. *Hivi leo tuna miaka siyo pungufu ya miaka kumi tano na tano*

Now today we are grown-up, we are no longer children of fifteen years old,

18. *Nimeshazaa mtoto MTAKA tena mke wangu ni mjamzito-zito*

I have already got a child MTAKA, moreover my wife is pregnant

19. *Leo hii waja kwangu kisa na mkasa nimeshakuwa **kizito-zito***

Today this is my situation, because I am in a relation

20. *Labda **umeditishwa** wataka nami uje unidatishe-tishe*

Perhaps you are already infected and you want me to infect me too

21. *Labda **umekanyaga miwaya** wataka nami nije niikanyage-nyage*

Perhaps you are infected with AIDS and you want me infect me too

Chorus

²⁰² -tuliza is used for *hakuna ngono ovyo*.

Verse 5.

22. *Fununu nimezipata-yakuwa wewe umeshaathirika-rika*

I have heard the rumours that you are already infected

23. *Ndiyo kisa wanilembu-lia ili nami nije athirika-rika*

Yes they wrote me the story that I would become infected too

24. *Nakuomba samahani-afadhari nije kufa kwa **mizuka-zuka***²⁰³

Excuse me, it is better that I die because of drugs

25. *Nasema **umechemsha-katu** kwangu zipu yangu haitofunguka*

I say it is impossible for me to start a relationship with you

Chorus

Verse 6.

26. *KIKWETE (RAIS) ametangaza kila mtu achunge*

KIKWETE (president) has announced that everybody has

27 *Maisha yake –yake- gonjwa ili ni hatari Lina-*

To take care of his life, the disease is a danger It

28. *weza likatimaliza sote-sote*

Can destroy us all-all

29. *Mfano ameutoa RAIS mzima ameenda akapima-pima*

The president has set an example in a healthy condition he has gone to have an examination

30. *Kwa nini mimi na wewe tusiende kwa hiari tukapima-pima*

Why do not we go voluntarily for a test,

Rap 3

Mapenzi Pipi ‘Love, Candy’

Chorus:

1. *Tusiendekeze Mapenzi kama pipi*

Let us not give in to our desires for love like candy

2. *Tusiendekeze Mapenzi kama **Beggej***

Let us not give in to our desires for love like candy

3. *Tusiendekeze Mapenzi kama Maji. Oho*

Let us not give in to our desires for love like water, oho,

4. *Ukimwi utatimaliza x2*

AIDS, will kill us x2

Verse 1

²⁰³ *mzuka* is elders gebruikt als ‘seduction’ here ‘seduction of drugs’.

5. *Kwa heshima na taadhimu naja mbele yenu kwa Saruti,*
With respect and dignity I come to you with a salute,
